# Nipashe

Jumapili Juni 2, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581695

www.twitter.com/nipashetz


www.ippmedia.com

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

JUMAPILI

LIKE & FOLLOW US

**Dk**. Mpango awa mbogo uchafu wa soko la Ilala



UKURASA 3

**JKCI** yazindua kitanda maalum kufuatilia mgonjwa akiwa nyumbani




UKURASA 5

**Walimu** wafikiwa na elimu kukwepa mikopo umiza, kausha damu

UKURASA 8

**City yavutiwa na Rodrygo**

UKURASA 22

## RIPOTI MAALUM

# Hivi ndivyo ulivyo ukwepaji wa kodi



Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata

• **Wafanyabiashara** waja na mbinu mpya, serikali yapoteza mabilioni... *Endelea ukurasa 4*



# Fursa tele ziara ya Rais Samia Korea

UK. 2

UKURASA WA 5

## MRADI BIL. 104/- KUPAISHA SEKTA YA MADINI



SERIKALI inakusudia kutekeleza mradi mkubwa wenye thamani ya Sh. bilioni 104 utakaotoa umeme wa uhakika kwa wawekezaji wa migodi ya madini katika wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro...

# Aliyedaiwa kuuawa na mke akiwa kwa hawara azikwa

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Mtafiti wa Kituo cha Kubadilishana Maarifa ya Kidunia na Maendeleo (GKED), Hyerin Byun kuhusu safari ya mafanikio ya Jamhuri ya Korea, alipotembelea kituo hicho, Seoul nchini humo, jana. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** **GAMONDI: HATUTARUDIA MAKOSA** UK.24

**MAONI,** UK.6

## Fursa tele ziara Samia Korea

**Na Salome Kitomari,** KOREA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amekamilisha siku moja ya ziara ya kikazi nchini Korea kwa kutembelea Kituo cha Kitaifa cha kubadilishana ujuzi na maendeleo Korea (GKED).

Rais Samia alianza ziara ya kikazi ya siku sita, alifika kwenye kituo hicho chenye historia ya teknolojia iliyotunzwa kidijitali na kupata maelezo ya namna walivyoweza kuhama na kufikia hatua kubwa.

**KUHUTUBIA MKUTANO**

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, akiwa mmoja wa viongozi walioambatana na Rais Samia katika ziara hiyo, alieleza sababu iliyofanya Rais Samia kuhutubia mkutano kati ya serikali ya Korea na wakuu wa nchi za Afrika.

Kadogosa alisema ni kutokana na uwekezaji mkubwa Tanzania uliofanywa kwenye miundombinu ikilinganishwa na nchi zingine. Alisema katika mkutano huo, Rais Samia atatoa maoni katika jopo la kuimarisha usalama wa chakula na madini.

Kadogosa alisema maelekezo ya Rais Samia kwa TRC ni kuhakikisha treni inaanza kazi ifikapo Julai 14, mwaka huu, kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro na ifikapo Julai 25, itaanza safari ya Morogoro kwenda Dodoma.

Ziara ya Rais Samia nchini Korea ni ya kimkakati kutokana na fursa nyingi zilizopo kwa Tanzania kwenye biashara, miundombinu na mazao kwa kipindi ambacho Korea inajitanua kufungua milango kwenda Afrika, kwamba biashara kati ya nchi hiyo na dunia, Afrika inaambulia asilimia moja pekee.

Ziara hiyo ambayo ya kikazi ni ya kwanza kwa miaka 26. Ya kwanza ilifanywa na Rais Mstaafu Hayati Benjamin Mkapa mwaka 1998 wakati mwaka 2006 Rais Mstaafu Jakaya Kikwete alikwenda kwenye mkutano.

Ziara za marais wa Jamhuri ya Korea kwa Afrika ni 11 ambazo walikwenda nchi mbalimbali zikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Ethiopia, Afrika Kusini, Nigeria na Kenya.

Jamhuri ya Korea ni ya 13 kwa uchumi duniani, inafungua masoko mapya kutokana na somo walilolipata wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa corona wakitegemea nchi za China, Japan na Russia ambako kulifungwa na malighafi kuchukua muda mrefu kufika.

**KWA NINI TANZANIA**

Tanzania ni ya pili Afrika kwa kupokea misaada na mikopo ya miradi nafuu kutoka Jamhuri ya Korea ikipokea Dola za Marekani bilioni 1.3. ya kwanza ni Misri inayopata Dola bilioni 1.6.

Tangu kuanza kwa uhusiano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea mwaka 1992, kwa miaka mitano misaada iliyopokelewa mwaka 2014-2020 ilikuwa ni Dola za Marekani milioni 733 ambazo zilitumika kwenye miradi ya ujenzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili tawi la Mlonganzila.

Miradi mingine ni Daraja la Maragarasi, Mradi wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), mradi wa umwagiliaji Zanzibar.

Mwaka 2021 hadi 2025 Tanzania ilitia saini miradi ya Dola za Marekani bilioni moja inayotekelezwa ambayo ni upimaji ardhi kwa dijitali, Chuo cha Teknolojia Kijiditali (DTI), Ujenzi wa Hospitali ya Miguni Zanzibar ya vitanda 600.

Pia kuna mradi wa Dola za Marekani milioni 230 wa kujenga upya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ambayo itakuwa ni maghorofa na kwamba ujenzi utaendelea, huku huduma zikiendelea na hadi mwaka 2030 utakuwa umekamilika.

Miradi mingine ni Zanzibar kitajengwa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano, Bandari ya Uvuvi Bagamoyo na Chuo cha Reli cha Kisasa, kwamba nyongeza ya mkopo wa Dola za Marekani bilioni 2.5.

Aidha, mikopo hiyo Tanzania itaamua miradi ya kutekeleza na kwamba riba yake ni asilimia 0.001 ukaaolipwa kwa miaka 40 na inalipwa baada ya miaka 25.

**KITAKACHOFANYIKA**

Katika ziara hiyo, Rais Samia atatia saini makubaliano katika maeneo mbalimbali ikiwamo mkataba wa mkopo mpya utakaoanza mwaka 2024 hadi 2028, ushirikiano kwenye madini ya kimkakati.

Katika eneo la madini Tanzania imejipanga kimkakati kwa kuongeza thamani ya madini ili kuhakikisha wananchi wananufaika. Eneo lingine ni kufungua uchumi wa bahari (uchumi wa buluu).

Katika ziara hiyo, Jamhuri ya Korea itatoa tamko la ushirikiano baina yake na Tanzania baada ya kujiridhisha na sifa za kisiasa na amani.



Waombolezaji wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa marehemu Ephagro Msele (43) aliyechomwa kisu na mkewe Beatrice Kwayu kwa tuhuma za kukutwa kwa mzazi mwenza, baada ya kufanyiwa ibada ya misa takatifu katika Parokia ya Bikira Maria Mtolewa Hekaluni Karanga, mjini Moshi jana. **PICHA: MARY MOSHA**

# Aliyedaiwa kuuawa na mke akiwa kwa hawara azikwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAMIA ya wakazi wa Mji wa Moshi na mikoa ya jirani, jana walijitokeza kuhitimisha safari ya mwisho duniani ya mfanyabiashara Evagro Msele (43), anayedaiwa kuuawa wiki iliyopita na mkewe wa ndoa, kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali mgongoni.

Baada ya kumkuta nyumbani kwa mwanamke mwingine aliyezaa nae.

Msele, aliuawa Mei 25 mwaka huu, majira ya saa 3:50 usiku na mtu anayedaiwa kuwa mkewe wa ndoa, Beatrice Elias (36), katika eneo la Pumuwani A, Kata ya Kirua Vunjo, wilaya ya Moshi, baada ya kumkuta nyumbani kwa mwanamke mwingine aliyezaa naye.

Wakati wa ibada ya maziko ake yaliyofanyika nyumbani kwake, Mtaa wa Katanini, Kata ya Karanga, Manispaa ya Moshji, Paroko wa Parokia ya Bikira Maria Mtolewa Hekaluni - Karanga, Padri Sarafinini Kilawe, alisema angekuwa na uwezo wa kuzuia kifo cha Msele, angesema roho yake (uhai wake) irudi duniani kwa sababu ya matoleo yake kanisani.

"Hata mimi si kuamini kama amekufa na ningekuwa naweza ningesema roho yake irudi kutokana na majitoleo yake katika kanisa, jamii na familia lakini kazi ya Mungu haina makosa, na yeye ndiye anayejua siku na saa yake, hivyo tujiweke tayari kila wakati.

Alisema katika miaka yake 43, amefanya kazi kubwa utadhani alikuwa anajua kifo chake, alionyesha upendo usio na mipaka; na nadhani ndio chanzo cha kifo chake. Mimi nimefanya nae kazi katika kama kiongozi kwenye parokia hii, natambua mawazo yake katika kujenga, kusuluhisha na kutafuta amani na tija kwa kanisa." alisema Padri Kilawe.

Msele, ameacha watoto saba, wawili wakiume na watano wa kike.

Padri Kilawe, alisema kila aliyepata taarifa za kifo hicho hakuamini kutokana na umri wake na mambo yake kwenye jamii ikiwamo upendo kwa jamii na kusaidia wahitaji.

Paroko huyo alisema Mei 24 mwaka huu (siku moja kabla ya kifo chake), walizungumza juu ya siku ya Juni 2 (leo) kuhusiana na maandalizi ya andamo la Sakramenti ya Ekaristi Takatifu.

Alisema yeye hawezi kutoa sifa za kumpamba na badala yake anaelezea hali halisi ya marehemu huyo na jamii inajua hilo.

Kiongozi huyo wa kiroho aliwataka wanaume na wanawake kutumia muda mwingi kuombea na kuacha maneno yasiyo na tija ili kuleta matokeo chanya katika ujenzi wa familia na vizazi vijavyo.

**KABLA YA KIFO**

Baadhi ya watu wa karibu na Msele, wameelezea tukio hilo kwamba Mei 25, mwaka huu, Beatrice baada ya kutoka kwenye maziko ya mama wa mfanyabiashara mwingine maarufu Kanda ya Kaskazini, alianza kumfuatilia mumewe kwa kificho kila alikokuwa akienda, akitumia usafiri wa bodaboda na baada ya mumewe kuegesha gari lake mahali, alikwenda nyumbani kwa mwanamke huyo aliyezaa naye.

Inadaiwa kuwa Beatrice alipofika nyumbani kwa mwanamke huyo, Kitongoji cha Pumuani A, alijificha getini na baadaye aligonga geti na mumewe ndiye aliyetoka kumfungulia.

Baada ya kukutana getini, yaliibuka mabishano kati yao, ndipo Beatrice alipofanikiwa kutekeleza tukio hilo.

Wiki iliyopita, kaka wa marehemu, Peter Msele, alisema mdogo wake alikuwa msibani jana (Jumamosi iliyopita), yeye na mkewe, baadaye alitoka kwenda kumfuata mwanamke aliyekuwa amezaa naye.

Alisema baada ya mkewe kujua kwamba mumewe anakwenda kwa mzazi mwenzake, alimfuata kimya kimya hadi nyumbani kwa mwanamke huyo.

"Jana mdogo wangu alikuwa kwenye msiba na mke wake, sasa baada ya kuzika akaondoka na kumuacha mke wake pale msibani na wakati huo, alikuwa amemfuata mwanamke ambaye amezaa naye huko Pumuani.

"Sasa mke wake akawa anamfuatilia, ikafika mahali akaacha gari njiani akapanda bodaboda kumfuata mume wake na huyu mama ni kama anapajua kwa huyo mwanamke aliyezaa na mume wake,"alisema Peter.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Pumuani A, Abrahaman Mnyanyembe, alisema baada ya kupigiwa simu kuwa kuna tukio la mauaji kwenye eneo lake, alifika haraka na kukuta mauaji hayo yamefanyika.

"Nilipigiwa simu jana usiku na wananchi wangu kuwa kuna tukio limetokea, kuna mtu anavuja damu nyingi kama kapigwa na chuma, niliamka haraka kwenda na kweli nilipofika eneo la tukio nilimkuta yule baba kalala chini na damu nyingi zinavuja.

"Niliwapigia simu polisi, wakafika eneo la tukio na wakati huo huyu mke wake (mtuhumiwa) yupo eneo la tukio, polisi walikagua na wakati wanachunguza mwili wa marehemu walikuta amechomwa kisu," alisema Mnyanyembe.

HABARI KITAIFA

# Mpango awa mbogo uchafu soko Ilala

**Na Gwamaka Alipipi**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameeleza kutoridhishwa na hali ya usafi katika soko la Ilala na kutoa siku saba kwa viongozi wa Jiji la Dar es Salaam kumaliza tatizo la majitaka yanayotiririka na kutoa harufu kali kwenye eneo hilo.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo jana aliposhiriki kufanya usafi wa kila Jumamosi katika soko hilo. Pamoja na mambo mengine aliwaagiza viongozi husika kufanya kazi kwa bidii ili limalizike haraka.

Katika shughuli hiyo, Dk. Mpango alijumuika na viongozi wakuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani inayoadhimishwa Juni 5, kila mwaka.

Akiwa sokoni hapo, Dk. Mpango alisema alipanga kwenda sehemu fulani (hakuitaja) kufanya usafi lakini ghafla usiku alibadilisha uamuzi na kwenda soko la Ilala kwa lengo la kushiriki usafi wa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.

"Suala la usafi ni jambo muhimu sana. Miji yetu isipokuwa safi na mvua ikinyesha tunaathirika na magonjwa kikiwamo kipindupindu. Lakini kuna adha kama hii harufu iliyonipokea nani anapenda hiyo?

"Labda niseme tu jana walitaka kunipeleka sehemu, nikawaambia hapana nataka kwenda kwa ndugu zangu wananchi wa kawaida. Nilipoambiwa Ilala nikasema sawa hapo nakwenda nyumbani, nakushukuru Mkuu wa Mkoa (Albert Chalamila) na mabadiliko yalifanyika usiku,"alisema.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Kiula Kingu, alimweleza Dk. Mpango mikakati ya taasisi hiyo ya kuondokana na tatizo hilo.

Kingu alisema wako mbioni kuanza ujenzi wa mabwawa ya taka ya kisasa maeneo ya Buruguni mchakato utakaochukua miezi 18. Pia, alisema mradi huo ukikamilika utapunguza changamoto hiyo, maeneo ya Ilala na Kariakoo.

"Lakini hiyo haizuii DAWASA kutekeleza jukumu la kuondoa majitaka, kwa sababu tumenunua magari makubwa ya kunyonya na kuondoa majitaka yanayosambaa katika maeneo haya.

"Tumeshaelekeza magari matatu na mashine kwa ajili ya kusukuma majitaka kwenda katika maeneo husika, lakini mpango mkubwa ni ujenzi wa mabwawa hayo yatakayochakata pia mbolea," alisema Kingu.

Hata hivyo, Dk Mpango alimtaka Kingu na timu yake kuchukua hatua za dharura kunusuru hali hiyo, akisema miezi 18 mbali na harufu hiyo inahatarisha maisha ya wananchi, ndipo alipomuuliza ampe muda gani kuondoa adha hiyo.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akifanya usafi katika Soko la Ilala, jijini Dar es Salaam jana,wakati wa maadhimisho ya Siku ya Usafi, kuelekea Siku ya Mazingira Duniani. Kushoto ni Naibu Spika wa Bunge na Mbunge wa Ilala, Mussa Azzan 'Zungu'. **PICHA: OMR**

Baada ya majadiliano ya muda mfupi, Dk. Mpango alitangaza kuwa Kingu ameomba apewe muda wa wiki moja kushughulikia hali hiyo, akisema ndani muda hataki kuona maji hayo yakitiririka.

Pia alimuagiza Chalamila kuipitia upya menejimenti ya fedha ya Soko la Ilala ili kujiridhisha kama fedha hizo zinakusanywa kwa ufanisi na kutumika kama ilivyokusudiwa.

"Nimeshangaa hata fedha inayokusanywa hapa haujui ajabu kweli, nina hofia zinaishia mahali hakikisheni fedha inayotakiwa kukusanywa kutoka kwa wananchi hawa inarudi kuwahudumia," alisema Dk. Mpango.

Hofu ya Dk. Mpango imetokana na swali lake alilouliza kwa uongozi wa Jiji la Dar es Salaam la kutaka kujua kiwango cha fedha kinachokusanywa kutoka katika soko hilo, lakini hakukuwa na majibu ya kuridhisha.


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

RIPOTI MAALUM

# Hivi ndivyo ulivyo ukwepaji kodi

**Na Maulid Mmbaga**

"UKIUZA toa risiti, ukinunua dai risiti." Ni msemo ambao ulizoeleka wakati wa uongozi wa awamu ya tano chini ya Hayati Dk. John Magufuli, ikiwa ni kusisitiza umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya taifa.

Msisitizo huo ulikuwa pia kwa ajili ya kudhibiti bidhaa za wizi na magendo kwa kuwa kutokuwa na risiti ya bidhaa husika iliyonunuliwa ni kosa kisheria na mhusika anaweza kukabiliwa na kifungo jela kwa kuwa na mali ya wizi.

Kuna msemo kwamba kadiri uhalifu au uovu unavyodhibitiwa, ndivyo wahusika wanavyobuni mbinu mpya katika kutimiza malengo yao. Hivyo ndivyo ilivyo sasa baada ya wajanja hao kubuni mbinu mpya ya kukwepa kodi kwa kutumia biashara ya mtandao.

Baadhi ya wafanyabiashara hao wametengeneza makundi sogozi ya mitandao ya kijamii ya WhatsApp, Instagram, Facebook kwa ajili ya kufanikisha biashara zao huku sehemu kubwa wakiwa hawatimizi matakwa ya kisheria ya kutoa risiti. Katika matangazo yao kwenye makundi hayo, wamekuwa wakionyesha bidhaa mbalimbali na bei huku wakisisitiza kwamba wanamfikishia mteja popote alipo bila gharama kwa mkoa husika.

Baada ya mteja kufikishiwa bidhaa aliyoichagua kupitia mtandaoni, anatakiwa kulipa fedha kulingana na bei waliyokubaliana kwa njia ya 'lipa namba' ya kampuni za simu za mkononi kama vile Vodacom, Airtel na Tigo lakini hakuna risiti inayotolewa kuonyesha uthibitisho wa ununuzi wa bidhaa hizo.

Mbali na biashara hiyo ya mtandao, wako wafanyabiashara wengine ambao huzunguka na bidhaa mbalimbali hususan vyombo vya nyumbani na umeme kama vile pasi na kupita nyumba kwa nyumba na kuuza kwa fedha taslimu au kwa mkopo na malipo kufanyika kwa muda maalum kwa mujibu wa makubaliano.

Uchunguzi uliofanywa na gazeti hili kwa wiki kadhaa, umebaini kukithiri kwa biashara hiyo huku serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikikosa mapato hasa kupitia kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ambayo ni asilimia 18 ya thamani ya bidhaa husika.

Kwa mujibu wa uchunguzi huo, baadhi ya wafanyabiashara hao wamekuwa wakiuza bidhaa mbalimbali ambazo bei kwenye mitandao hiyo zinaonyesha ni kati ya Sh. 100,000 na Sh. milioni 2.5. Miongoni mwa bidhaa hizo ni mashine za kukamulia juisi, friji, runinga za saizi tofauti, redio (home theatre), vyombo vya chakula kama vile sufuria na seti ya chakula (dinner sets).

Hatua hiyo, kulingana na uchunguzi uliofanyika, inaisababishia serikali kukosa mapato yatokanayo na kodi kwa wastani wa sh. 18,000 (bidhaa ya thmani ya chini) hadi Sh. 450,000 kwa kila bidhaa kwa zile zenye thamani ya juu.

Kutokana na kuwapo kwa biashara hiyo, uchunguzi umebaini kwamba kuna baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakiendesha shughuli zao bila kutoa risiti baada ya mauzo jambo linalosababisha aliyenunua kushindwa kurudisha bidhaa husika kama ni mbovu.



Pia imebainika kwamba asilimia kubwa ya wafanyabiashara hao hawatumii au hawana kabisa mashine za EFD jambo linaloashiria kwamba hawatoi risiti baada ya kumuuzia mteja bidhaa licha ya kwamba ni kinyume cha maelekezo ya TRA.

Joseph Lymo, mmoja wa wafanyabiashara wanaomiliki maduka na kuuza kwa njia ya mtandao, alipohojiwa na gazeti hili, alikiri kwamba kuna baadhi wanakwepa kutoa risiti wanapomuuzia mteja bidhaa lakini sio wote.

"Hilo jambo inawezekana lipo lakini ni baadhi na wanaofanya hivyo ni kwa lengo la kukwepa zile gharama zinazoenda TRA. Tatizo liko pale mtu anapoona biashara imekuwa ngumu, fedha anazoingiza hazikidhi mahitaji yake. Mwisho anaona ni bora afanye hivyo akidhani kwamba ndiyo njia ya kumuongezea kipato," alisema.

Frank Chuwa, muuzaji wa viatu kwa njia ya mtandao, alisema hana ofisi maalumu ya kuendesha biashara zaidi ya mtandaoni ndio maana hana mashine ya EFD na kwamba endapo mteja wake atahitaji huwa anamwandikia ya mkono na kumtumia kama picha baada ya kufanya malipo.

"Sisi bado ni wajasiriamali wa chini tunauza kwa oda maalumu. Naweka bidhaa mtandaoni mtu akitaka naenda Kariakoo kumchukulia na siwezi kuwa na mashine kwa sababu sina fremu. Mteja akilazimisha juu ya risiti tunamwandikia ya mkono basi," alisema Chuwa.

**WANANCHI WANASEMAJE**

Mariam Awadhi, mkazi wa Tabata, alisema amekuwa akinunua bidhaa mtaani kwa muda mrefu lakini hakuwahi kupewa risiti na kwamba siku moja alijaribu kutaka apewe lakini mwenye bidhaa alidai kuwa mashine ya EFD imeharibika, hivyo atamuandikia ya mkono.

Licha ya kutopewa risiti lakini wauzaji wengine sio waaminifu kwakuwa baadhi ya bidhaa wanazouziwa hazidumu, akibainisha kuwa kinachosababisha wengi kukimbilia kuzinunua ni kwa sababu ya unafuu wa bei, hivyo haoni umuhimu wa kukulazimisha apewe risiti baada ya kununua bidhaa.

"Nafikiri wengi hawana pia uelewa wa umuhimu wa kuhakikisha anapewa risiti baada ya kununua na wafanyabiashara wengi wanalifahamu hilo ndiyo maana na wao hawalipi uzito suala hilo kama wale wanaouzia dukani. Lakini pia suala la kudai kwamba mashine imeharibia tunakutana nalo sana," alisema.

Fadhili Mlanga, alidai kwamba hana uhakika kwamba TRA inawatazama sana wafanyabiashara hao, akieleza kuwa suala la kutokutoa risiti kwao limekuwa la kawaidi kwa sababu wengi wanazungusha bidhaa zao mitaani lakini hawabebi mashine hizo.

"Sijawahi kuona hata siku moja wakiwa wameshika ile mashine. Kama wanakuwa nazo basi itakuwa wanazificha kwa sababu wanajua kwamba ukiona utawaambia wakutolee risiti.

Watu wengi wanapuuzia lakini risiti ni muhimu kwa sababu inaweza kusaidia. itaani kuna mambo mengi mtu anaweza kuja akuambie hucho kitu umeiba, katika hali hiyo kama huna risiti unaweza kuingia matatizoni," alisema Mlanga.

**KAULI YA TRA**

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Hudsom Kamoga, akizungumza na gazeti hili kuhusu suala hilo, alikiri kwamba lipo na kutahadharisha kuwa kufanya biashara yoyote bila kutoa risiti ni kosa kisheria kwa muuzaji na mnunuzi.

"Mtu yeyote anayeuza bidhaa na hata kununua bila risiti anajiweka katika hatari kwa sababu anavunja sheria na kuikosesha serikali mapato. Nisisitize kwamba anayeuza bidhaa anawajibika kisheria kutoa risiti na anayenunua ana wajibu wa kudai risiti.

"Mnunuzi pia atambue kuwa kushindwa kupewa risiti ya bidhaa kulingana na thamani aliyonunulia ni kosa kisheria na anajiweka katika mazingira magumu hata kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Anaweza akawa ananunua bidhaa bila kujua kuwa mzigo anaonunua ni wa wizi au amewekewa mtego baada ya muda anafanyiwa 'search' (msako) na kukamatwa kwa sababu hana risiti. Utetezi wake utakuwa nini zaidi ya kufikishwa kwenye vyombo vya sheria," alisema.

Kamoga alitoa tahadhari kwa wananchi kwamba kununua bidhaa bila kutoa risiti kunasababisha wakose huduma mbalimbali kama vile afya au kupata zikiwa duni wakati mfanyabiashara anajinufaisha kwa kukwepa kodi ambayo anaitoa mwananchi na yeye ni wakala wa TRA katika kukusanya VAT.

"Inapotokea huduma ni mbovu au duni wanailalamikia serikali wakati chanzo ni wao wenyewe (wananchi). Mwenzake akiugua yeye na familia yake watakwenda India kutibiwa wakati mnunuzi ataishia zahanati au hospitali za hapa nchini ambako pia atalalamika kuwa huduma ni duni," alisisitiza.



# Mradi bil. 104/- kupaisha sekta ya madini

**Na Ashton Balaigwa,**
IFAKARA

SERIKALI inakusudia kutekeleza mradi mkubwa wenye thamani ya Sh. bilioni 104 utakaotoa umeme wa uhakika kwa wawekezaji wa migodi ya madini katika wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro.

Aidha, serikali inatarajia kutangaza wakati wowote wilaya za Ulanga, Malinyi na Kilombero kuwa ni mkoa wa shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutokana na umuhimu maeneo hayo katika kuzalisha mazao mbalimbali yanayosaidia kukuza uchumi.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema hayo mjini hapa wakati akizindua mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme wa uhakika kwa wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga.

Kituo hicho kimejengwa na serikali ya Tanzania kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa ushirikiano na Umoja wa Ulaya (EU) kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Ulaya (EDF) kwa gharama ya Sh. bilioni 24.59 ikiwa ni kuunga mkono jitihada za serikali za kuondoa umasikini katika kuendeleza kilimo.

Naibu Waziri Mkuu alisema Ulanga ni moja ya wilaya zilizobarikiwa kuwa na madini ya aina tofauti yakiwamo ya Kinywe, vito (spinal), hivyo wawekezaji wengi wamekuwa wakijitokeza kuwekeza lakini changamoto kubwa imekuwa umeme wa uhakika.

"Tunataka kujenga mradi mkubwa wa zaidi ya Sh, bilioni 104 ambao utakuwa unajitegemea kwa kupeleka umeme wa uhakika katika migodi yetu ili kuvutia wawekezaji kutoka nje na tunafanya hivi kwa uzito mkubwa," alisema.

Kuhusu manufaa ya mradi huo, Dk. Biteko alisema utasaidia upatikanaji wa umeme wa uhakika katika wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi ambazo zilikuwa na tatizo la a kukatika kwa umeme zaidi ya saa nane kwa siku. Alisema baada ya mradi huo kukamilika, umeme unakatika kwa dakika 46 pale yanapofanyika matengenezo.

Alisema kukamilika kwa mradi huo pia kutawezesha sehemu za biashara na viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo 54 kupata umeme wa uhakika na kufanya ukusanyaji wa mapato kwa TENESCO kuongezeka.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Jones Olotu, alisema wameamua kujenga kituo cha kupoza umeme Ifakara kutokana na wilaya hizo kuzalisha kwa wingi mpunga pamoja na miwa ambayo husaidia kukuza uchumi wa nchi.

Alisema kutokana na umuhimu wake kwa wilaya hizo , tayari vijiji 110 vilivyoko eneo la mradi vimeshapatiwa umeme na vilivyobaki 180, baada ya miaka miwili navyo vitakuwa na umeme.

Naye Balozi EU nchini, Christine Glau, alisema umoja huo utaendelea kuisaidia serikali ya Tanzania katika kutekeleza miradi yake mbalimbali yakuondokana na umasikini.

Alisema kituo hicho ni miongoni mwa vituo 14 ambavyo wanatarajia kuvijenga hapa nchini ambavyo vitakuwa na thamani ya Sh. bilioni 600.

Balozi huyo alisema kuwapo kwa umeme wa uhakika sasa utasaidia wakulima wa mpunga kuuza mchele badala ya kuuza mpunga kwa bei ya chini.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema wilaya hizo tatu za Kilombero, Ulanga na Malinyi kwa muda mrefu zilikuwa zikikabiliwa na changamoto ya umeme licha ya kuwa kinara wa uzalishaji wa mpunga na miwa.

Alisema asilimia 70 ya sukari inayozalishawa nchini inatoka mkoa wa Morogoro ambao una viwanda vinne vya kuzalisha sukari pamoja na kuzalisha mpunga.



Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi (kushoto) akipokea zawadi ya picha ya Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa niaba yake, kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (MISA-TAN), James Malenga, jijini Dar es Salaam juzi, iliyotolewa na taasisi hiyo, katika Kongamano la Tafakuri ya Mwaka la Uhuru wa kujieleza, kutokana na Rais kuimarisha uhuru wa habari na kujieleza hapa nchini. Kulia ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Elizabeth Riziki. **PICHA: MARCO MADUHU**

# JKCI yazindua kitanda cha kufuatilia wagonjwa kidijitali wakiwa nyumbani

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na Sakaar Healthtech kutoka India, imezindua kitanda maalumu 'Dozee', kinachotumia teknolojia mpya ya akili mnemba (AI), kufuatilia hali ya mgonjwa akiwa nyumbani.

Akizindua kitanda chenye teknolojia hiyo jijini Dar es Salaam juzi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema Afrika kuna rasilimali za kutosha ingawa changamoto ni namna ya kuzifanya zirahisishe maisha.

Alisema bara la Afrika, husan kusini mwa jangwa la Sahara, ambako kuna idadi kubwa ya Mangonjwa Yasiyoambukiza (NCD), kunahitaji kuwapo mbinu za kukabiliana nayo, ikiwamo vifaa tiba.

"Serikali imejitahdi kuwekeza katika sekta ya afya na tunaona namna JKCI inavyoongeza uwezo wa shughuli zao. Ukweli ni kwamba magonjwa yapo, kuhakikisha tunakabiliana nayo, kwa kuwa na teknolojia kama hii,

"Kwa Afrika hii ni teknolojia ya kwanza na imezinduliwa hapa Tanzania. Huduma hii itawezesha mtaalamu kumfuatilia mgonjwa aliye nyumbani. Napongeza JKCI na kampuni iliyobuni kifaa hiki cha dozee," alisema Chalamila.

Alisema pamoja na teknolojia kukua, kuna haja ya Watanzania kuendelea kufanya mazoezi kila mara, ikiwamo kufanya uchunguzi wa afya zao, ili kubaini hali zao kiafya.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema kitanda hicho kinamsaidia muuguzi aliyepo hospitalini, kumfuatilia mgonjwa aliyepo nyumbani, kubaini hali ya presha, mfumo wa upumiaji na oksijeni.

"Kumfutilia mgonjwa akiwa nyumbani, kwa kutumia akili mnemba itapunguza gharama, muda, lakini pia iwapo hali ya mgonjwa hairidhishi, muuguzi atamshauri msimamzi wa mgonjwa kumrejesha hospitali kwa matibabu

"Tunashukuru waanzilishi wa dozee, teknolojia ambayo ni muhimu kwetu JKCI. Teknolojia hii inatumika nchi tatu duniani. India yenyewe, Marekani na Tanzania sasa itakuwa ya tatu," alisema Dk. Kisenge.

Kaimu Balozi wa India nchini, Manoj Verma, alisema nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania, hususan kwenye sekta ya afya, kama vile upatikanaji wa vifaa tiba na dawa.

# Juhudi zafanywa kutafuta masoko bidhaa nje ya nchi

**Na Joyce Lameck**

SERIKALI imesema inafanya jitihada ya kutafuta masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini ili ziwafikie watumiaji nje ya nchi, hali itakayochochea ukuaji wa uchumi.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara kutoka Wizara ya Viwanda na Maendeleo, Sekilo Manongi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha wajasiriamali wanawake kusajili biashara zao katika msimbomilia (barcode), iliyoandaliwa na kampuni ya GS1 Tanzania

Alisema serikali inafanya jitihada kutafuta masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuwafikia watumiaji nje ya nchi kwa ukubwa ili kukuza uchumi.

Manongi alisema wamefanya hivyo ili kuendana na teknolojia katika kufanya biashara.

Pia alisema ili kuitambulisha biashara, ni lazima iwe na msimbomilia yenye namba 260, hivyo aliwataka wanawake waunganishe biashara zao kwenye msimbo huo, ili kuweza kukuza biashara na hata uchumi wa taifa kwa ujumla, pia kuendana na teknolojia.

"Historia ya biashara yako huwezi kuirekodi yote na kufanya mtumiaji aamini kuwa ni bidhaa nzuri, ila kwa kurahisisha unaweza kufanya hivyo kwa kutumia msimbo kama kitambulisho kizuri cha biashara yako, kwani huwezi kuikwepa katika biashara, kwamba teknolojia inakuwa kwa kasi." alisema Manongi.

Mkurungezi Mtendaji wa GS1 Tanzania Barcode, Fatuma Kange, alisema wameandaa mpango maalumu kwa wanawake wajasiriamali 18,300 nchini kwa kuwachukua 100 katika kila wilaya ili kutekeleza mpango huo.

Hata hivyo alisema wameamua kushuka kwenye halmashauri ili kuwafikia wanawake walioko vijijini ambao wengi wao wanazalisha bidhaa zao lakini hawana masoko ambayo yanawasaidia katika kujikwamua kiuchumi.

Fatuma alisema gharama ya kulipia msimbo ni Sh. 75,000, ukilinganisha na bei ya awali iliyokuwa Sh. 230,000, kwamba wanaamini wafanyabiashara wataweza kulipia na kuipata kwa urahisi.

Pia, alisema kilele cha kampeni hiyo zitafanyika Oktoba 15, mwaka huu.

Mmoja ya wajasiriamali waliohudhuria mkutano huo, Husna Iddi aliishukuru GS1 kwa mpango huo maalumu akisema kuanzia sasa wataweza kufanya biashara kwa ukubwa tofauti na awali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukwepaji wa kodi wa aina hii katu usionewe huruma

**RAIS** wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, baada ya kuingia madarakani, alisisitiza ulipaji wa kodi kwa wafanyabiashara na kuapa kuwa asingekuwa na msamaha na watu wanaokwepa kodi. Alikwenda mbali zaidi kwa kusema wakwepaji wa kodi ni maadui wakubwa wa maendeleo.

Kiongozi huyo aliziishi kauli zake hizo na kuwataka wafanyabishara, kundi ambalo ndilo hutuhumiwa kuwa wakwepaji wakubwa wa kodi, wanapofanya shughuli zao wahakikishe wanatoa risiti. Pia aliwasisitiza wananchi wanaponunua bidhaa kwa wafanyabiashara wadai risiti inayoonyesha kiasi halali cha fedha walichotumia kununulia bidhaa husika.

Aidha, ili kuhakikisha wauzaji na wanunuzi wa bidhaa husika wanatekeleza hilo, alianzisha usemi kwamba "Ukiuza Toa Risiti, Ukinunua Dai Risiti" na katika kutekeleza hilo, alisisitiza matumizi ya mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD).

Hatua hiyo ilisababisha makusanyo yatokanayo na kodi kuongezeka na hatimaye serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Sambamba na matumizi ya mashine hizo kwa wafanyabiashara, serikali ilianzisha mfumo wa ukusanyaji mapato serikalini na mamlaka za serikali za mitaa, kutumia mashine za aina hiyo (POS) na malipo kwa njia ya mtandao ili kudhibiti ufujaji wa fedha za umma.

Katika uhalisia wa maisha, wahalifu au wakiukaji wa sheria ambao kwa kufanya hivyo hunufaika, hubuni mbinu mpya za kuendeleza maovu au kutenda mambo ambayo ni kinyume cha sheria.

Pamoja na nia hiyo nzuri ya serikali kuhakikisha wafanyabiashara wanalipa kodi kama inavyotakiwa, baadhi ya wafanyabiashara wameibuka na mbinu mpya ambayo inasababisha serikali kushindwa kukusanya mapato kwa mujibu wa malengo inayojiwekea kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania. Mbinu hiyo ni ya matumizi ya mitandao ya kijamii katika kufanya biashara ya bidhaa mbalimbali.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe Jumapili kwa wiki kadhaa, umebainisha kwamba biashara hiyo ya mtandao inaenea kwa kasi na mbinu wanayotumia ni kumzidishia mteja bidhaa aliyochagua popote alipo na kufanya muamala kwa njia ya simu bila kupewa risiti. Licha ya njia hiyo, kuna baadhi ya wafanyabiashara wanabeba bidhaa kwenye magari na kupita nyumba kwa nyumba kisha kuuza ama kwa fedha taslimu au mkopo na mteja kulipa kidogo kidogo kwa muda waliokubaliana.


Aina hii ya biashara imesababisha madhara kwa serikali kwa kukosa mapato stahiki ambayo yangetokana na kodi kwa kuuza bidhaa hizo. Baadhi ya wananchi waliouziwa bidhaa hizo wamekiri kwamba wanapofikishiwa bidhaa ofisini au nyumbani, wanatakiwa kufanya malipo kwa 'lipa namba' ya mtandao wa simu na matokeo yake hawapewi risiti. Mbinu hiyo ya wafanyabiashara hao kuuza bidhaa bila kutoa risiti, serikali inakosa kiasi gani cha mapato? Mfano mfanyabiashara anauza friji kwa Sh. 1,200,000 kiasi cha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ambacho ni asilimia 18 ni Sh. 216,000 na mashine ya kukamulia juisi ambayo inauzwa kwa Sh. 120,000 kiasi cha kodi kinachokwepwa ni Sh. 21,600.

Jambo la kujiuliza ni je, kwa biashara za namna hiyo serikali inakosa mapato kwa kiasi gani ambayo kiuhalisia, wafanyabiashara hao wanakwepa kodi inayolipwa na wananchi kwa kuwa wao ni mawakala wa TRA katika kukusanya VAT.

Wafanyabiashara hao, licha ya kuisababishia serikali hasara ya mabilioni ya shilingi kwa kukwepa kodi, wanajinufaisha kupitia kodi halali za Watanzania. Matokeo ya ukwepaji kodi huo ni kwamba mwananchi wa kawaida atakosa huduma bora kama vile afya akienda katika kituo cha kutolea huduma za afya cha serikali wakati mkwepaji kodi huyo akipata tatizo la afya, atakimbilia nje ya nchi kupata matibabu bora au katika hospitali binafsi nchini.

Kwa ujumla, ukwepaji kodi huu usipewe nafasi na njia pekee ya kutokomeza ni kwa wananchi kushirikiana na TRA katika kutoa taarifa kuhusu watu wa aina hii. Vyombo vya usalama na taasisi za utekelezaji wa sheria zishirikiane na TRA katika kupambana na uvunjaji huu wa sheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wananchi toeni ushirikiano kuboresha daftari la wapigakura

Na Sabato Kasika

**JULAI** Mosi mwaka huu, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), itaanza kazi ya kuboresha daftari la kudumu la wapigakura nchi nzima, ikilenga kuandikisha wapigakura wapya 5,586,422.

Idadi hiyo ya wapigakura inatajwa kuwa ni sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,699 ambao wamo katika daftari hilo baada ya kufanyiwa uboreshaji mwaka 2019/20.

Uboreshaji huo utaanzia mkoa wa Kigoma ambako tume inatarajia kuandikisha wapigakura 224,355 katika uboreshaji huo utakaozinduliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Julai Mosi, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Ramadhani Kailima, katika zoezi hilo nchi nzima, wapigakura 4,369,531 wataboresha taarifa zao na wengine 594,494 kuondolewa kwenye daftari hilo.

Sababu za kuondolewa kwao katika daftari hilo, zinaelezwa na mkurugenzi huyo kuwa ni kukosa sifa za kuendelea kuwapo kwenye daftari, na kwamba baada ya uboreshaji, inatarajiwa kuwa daftari hilo litakuwa na wapigakura 34,746,638.

Aidha, katika uboreshaji huo wa daftari la wapigakura, mkurugenzi anasema, kutakuwa na vituo 40,126 na kati ya hivyo, 39,709 ni vya Tanzania Bara na 417 ni vya Zanzibar.

Nikirejea kwenye hoja yangu, ni kwamba, kwa kuwa tume imeshatoa ratiba ya uboreshaji huo, ninadhani ni vyema watu wenye sifa wakajiandaa kushiriki katika zoezi hilo.

Hatua hiyo itasaidia kuwafanya waweze kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa Oktoba mwaka huu, hata uchaguzi mkuu wa 2025.

Kwa maana hiyo, wananchi wajiandae kutoa ushirikiano kwa watumishi wa tume ili kazi hiyo ifanyike kwa ufanisi maeneo yote ya nchi ili kupata idadi mpya ya wapigakura iliotangazwa na tume.

Uboreshaji pia utahusu kutoa fursa kwa wapigakura walioandikishwa awali na ambao wamehama kutoka mkoa au wilaya moja kwenda nyingine kuhamisha taarifa zao.

Uhamisho huo ni kutoka kata au jimbo waliloandikishwa awali, hivyo ni vyema makundi yote yanayolengwa, katika uboreshaji huo yakajitokeza kwa wingi ili asiwepo mwenye sifa atakaekosa kuandikishwa.

Hatua hiyo itakwenda sambamba na kutoa fursa kwa wapigakura walioandikishwa kurekebisha taarifa zao ikiwamo majina na zingine, kutoa kadi mpya kwa wapigakura waliopoteza kadi au kuharibika.

Nimejaribu kukumbushia hilo, kwa sababu baadhi ya Watanzania wana kawaida ya kutozingatia mambo ya msingi ambayo yanahusu hata maisha yao likiwamo hilo la kushiriki katika uchaguzi.

Wapo baadhi huwa hawashiriki katika uchaguzi, wakidai kuwa wao siasa haiwahusu, lakini wanasahau kuwa siasa ndio inayoamua maisha yao, kutokana na kwamba viongozi wa nchi hupatikana kupitia siasa.

Kutokana na mawazo hayo, wengine huwa hawashiriki kwenye uchaguzi, lakini akichaguliwa kiongozi ambaye huenda akashindwa kuongoza, huwa wanakuwa wepesi kulaumu kwa nini amechaguliwa.

Wanatoa lawama bila kujali kuwa nao wamechangia kumweka madarakani kiongozi wanayemlalamikia.

Kwa nini? Kwa sababu mtu kama ana sifa ya kupiga kura halafu hataki kushiriki uchaguzi, maana yake ni kwamba anachangia kumfanya yule asiyemtaka ashinde.

Nirudie kwamba wananchi watoe ushirikiano kwa watumishi wa tume ili iweze kufanikiwa kuwafikia walengwa wote waweze kushiriki katika uchaguzi wa mwaka huu na wa 2025.

Bila kufanya hivyo, itakuwa ni sawa na kutotimiza haki yao ya kuchagua na kuchaguliwa na mwisho wake ni kubaki na kulalamika tu kwamba waliopo madarakani hawafai kuongoza na kumbe wasiojiandikisha au wasiojitokeza kupiga kura ndio chanzo cha tatizo.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Hali ya kuchagua, kuchaguliwa irejeshwe kwa wananchi



Pascal Mayalla

HALI ya kuchagua, kuchaguliwa irejeshwe kwa wananchi

NAOMBA kuanza makala ya leo kwa nukuu kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan aliyosema: "Mabadiliko katika sheria zetu za uchaguzi yataleta ushindani wa haki na kuwapa watu fursa ya kuwachagua wawatakao kuwaongoza,"

Hii ni nukuu ya Rais Samia katika andiko lake la miaka 30 ya Vyama Vingi nchini Tanzania. Maneno hayo ni makubwa sana na yenye maana kubwa kwa sababu yanahusu kuwapa watu fursa ya kuwachagua wawatakao.

Uhuru wa watu kuwachagua viongozi wanaowataka ndiyo haki ya tatu ndani ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977. Haki kuu ya kwanza ni haki ya uraia, ya pili ni haki ya kuishi na ya tatu ni ya kuchagua na kuchaguliwa kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 5 na Ibara ya 21 ya katiba hiyo.

Haki hii ina sharti moja tu la umri wa miaka 18 kupiga kura, umri wa miaka 21 kuchaguliwa diwani au mbunge na miaka 40 kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungabno wa Tanzania (JMT).

Hakuna sharti la kulazimishwa kuwa mwanachama wa chama cha siasa. Kilichofanyika kuchomekea sharti la mgombea kudhaminiwa na chama cha siasa. Ndani ya Katiba yetu ni uhuni na ubatili tu uliofanyika na Mahakama Kuu iliisha ubatilisha ubatili huo.

Kiongozi yeyote anapoandika au anapohutubia, kuna mambo mawili kwenye andiko lake au hotuba yake. Mosi, kati ya andiko la kiongozi kuna vitu ni maono, mawazo, maneno na maandishi ambayo yeye mwenyewe kutoka moyoni mwake, kichwani mwake, mawazoni mwake, yaani ni yeye mwenyewe halisi.

Pili, viongozi wana wasaidizi ambao huwa wanawaandikia nini cha kusema (talking notes) na kwa Rais wa nchi, ana wasaidizi hotuba ambao wanamwandalia nini cha kusema kwa kumwandikia, kisha Rais anapitia kile alichoandikiwa lakini si chake. Anaweza kuongeza chake au kupunguza na ndipo anakuja kuhutubia au kutoa andiko.

Wakati akihutubia, tukisikia kila Rais anachosema kwenye hotuba yake, tunahesabu kila kilichosemwa ni Rais kusema. Msikilizaji huwezi kujua kipi ni chake mwenyewe na kipi ni ameandikiwa tuu lakini si chake.

Hii pia hutokea kwa wasomaji wa habari kwenye TV zote na redio zote. Watazamaji na wasikilizaji wanamwona mtangazaji na wanamsikiliza mtangazaji. Wanajua hizo habari wametangaziwa na mtangazaji fulani, wanajua ni mtangazaji huyo ndiye anajua habari hizo, kumbe hawajui kazi ya mtangazaji wa habari ni kutangaza tu habari alizoandikiwa na wengine. Yeye kazi yake ni kusoma tu.

Vivyo hivyo kwenye hotuba za viongozi, kuna viongozi wanasoma tu hotuba walizoandikiwa na wengine lakini si mawazo yao, si maneno yaov lakini ni matamshi yao.

Kama nilivyosema kwenye habari, mtangazaji unaandikiwa kisha unapewa kuipitia habari hiyo. Kwa Radio Tanzania (RTD) taarifa ya habari ni dakika 10, mtangazaji unatakiwa kuipitia nusu saa kabla, ili uielewe na unaposoma, unasoma kitu unachokijua.

Kitendo cha kuichukua habari ambayo hujaiandika, ukaipitia na kuisoma kama vile umeiandika wewe kinaitwa 'presence' kwa lugha ya Kiingereza. Ndiyo maana watangazaji huitwa 'presenters', kazi yao ni ku-present tu.

Kuna wakati msomaji wa habari unapitia habari usiyoielewa, unapaswa uulize, ili usisome kitu usichokielewa. Lakini katika mitikasi hii na ile, kuna siku mtangazaji unakuwa umechelewa kupitia Habari kabla, hivyo unasoma tu kwa uzoefu, hata ukikutana na kitu usichokielewa, unakisoma hivyo hivyo kilivyoandikwa na wasikilizaji na watazamaji watasikia tu na kuelewa.

Lakini kwa watu makini na kitu kinachoitwa 'graphology', wao watam- note mtangazaji anajiumauma ulimi, hivyo unajua tuu huyu mtu hajapitia hiyo habari, hivyo anasoma kwa uzoefu tu. Anasoma kitu asichokijua, anasema kitu alichoandikiwa lakini hakijui.

Vivyo hivyo hutokea kwenye baadhi ya hotuba za viongozi. Anakuwa ameandikiwa kitu asichokijua. Anapitia hotuba, kisha anahutubia kitu asichokijua.

Maneno hayo ya Rais Samia kwenye andiko lake ni maneno makubwa, mazito sana na mimi nikayaandikia makala kwenye safu yangu gazeti za Jumapili ya Julai 10, 2022 yanye kichwa cha habari , "Rais Samia Akitekeleza Hili, Hakika Tanzania Itabarikiwa".

Sasa sheria mpya ya uchaguzi imeshatungwa ila sheria bado ina ubatili ule ule tunaoupigia kelele. Hali hiyo inayonifanya kuanza kujiuliza hivi maneno haya "Mabadiliko katika sheria zetu za uchaguzi, yataleta ushindani wa haki na kuwapa watu fursa ya kuwachagua wawatakao kuwaongoza?"

Je, ni maneno ya Rais Samia mwenyewe au aliandikiwa? Je, hii sheria mpya ya uchaguzi, yenye ubatili ule ule, italeta vipi ushindani wa haki wakati Rais Samia ameahidi "kuwapa watu fursa ya kuwachagua wawatakao kuwaongoza"

wakati sheria mpya ya uchaguzi, watu bado hawana haki ya kuwachagua viongozi wanaowataka, bali wanalazimishwa kuwachagua viongozi walioptishwa na vyama vya siasa na si viongozi wanaowataka?

Tafsiri ya alichokisema Rais Samia na kilicholetwa kwenye sheria mpya ya uchaguzi ni vitu viwili tofauti. Kwa sababu muda bado tunao, nashauri hili liangaliwe ili sheria yetu ya uchaguzi iwe ya haki kweli kama Ibara ya 5 na 21 za katiba zinavyosema.

**Wasalaam**
**Paskali**
**+255 754 270403**

# Walimu kingereza wapewa mbinu ufaulu

**Na James Mwanamyoto,**
KARAGWE

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu Dk. Charles Msonde, amewapa mbinu walimu wa somo la Kiingereza katika ufaulu wa somo hilo.

Amesema mbinu ya kufikia azma hiyo ni kufundisha kwa umahiri ili kuwawezesha wanafunzi kupata ufaulu mkubwa katika masomo yote ya mtihani wa kidato cha nne, ikizingatiwa kuwa Kiingereza ndiyo lugha rasmi ya kufundishia.

Dk. Msonde alitoa wito huo juzi kwa walimu wote wa sekondari nchini, wakati wa vikao kazi vyake na maofisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu katika halmashauri za Wilaya ya Misenyi na Karagwe mkoani Kagera.

"Walimu zingatieni kufundisha Kiingereza kwani wanafunzi wakiwa na umahiri wa kuongea, kusoma na kuandika lugha ya kiingereza watapata ufaulu mzuri katika mtihani wa kidato cha nne, na hakutakuwa na divisheni ziro," alisema.

Dk. Msonde alisema hivi sasa walimu wanapaswa kuwa vitani katika kuleta mapinduzi ya elimu nchini, hivyo ufundishaji wa mazoea hauna nafasi katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita ambayo ina dhamira ya dhati ya kuboresha elimu kwa masilahi na manufaa ya taifa.



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde akisikiliza umahiri wa kuongea kiingereza wa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Bugene, alipoitembelea shule hiyo, wilayani Karagwe, mkoani Kagera juzi, ili kukagua miundombinu inayojengwa. **PICHA: TAMISEMI**

"Haiwezekani mtoto afundishwe na mwalimu kiingereza mwaka mzima alafu ashindwe hata kutamka neno la kiingereza 'uncle'. Kamwe haiwezekani ndiyo maana walimu mnapaswa kuingia vitani ili kutatua changamoto hii ya lugha ya Kiingereza," alisisitiza.

Msonde aliongeza kuwa katika elimu ya sekondari, lugha rasmi ya kufundishia ni Kiingereza, hivyo walimu wanapaswa kuitumia kuwafundisha watoto mpaka waelewe kwa kuwa mkakati wa kuboresha elimu umemlenga mtoto ili apate ujuzi kama ulivyoainishwa kwenye mtaala.

Dk. Msonde amehitimisha siku ya tatu ya ziara yake mkoani Kagera kwa kufanya vikao kazi na maafisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu katika halmashauri za wilaya za Misenyi na Karagwe na kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi hao.

# TASAF yapongezwa ujenzi wa madarasa

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

WANANCHI wa Kijiji cha Chingulungulu, Tunduru mkoani Ruvuma, wameupongeza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kuwajengea madarasa matatu.

Wamesema hatua hiyo ni juhudi za serikali za kusogeza huduma kwa wananchi na kuwapunguzia adha ya kusafiri umbali mrefu kufuata elimu.

Walitoa pongezi hizo juzi kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe kuhusu namna walivyoyfaidika na TASAF.

Mmoja wa wananchi hao, Hamisi Mohamed, alisema kabla ya ujenzi huo watoto wao walikuwa wakisafiria umbali mrefu kwenda katika Shule ya Msingi Chingulungulu na sisi kwa sisi ambazo zipo zaidi ya kilometa sita.

Naye Katibu wa Usimamizi wa Mradi huo, Asina Joseph, alisema pamoja na mambo mengine aliwapongeza wananchi wa kijiji hicho kwa ushirikiano waliouonesha wakati wote wa ujenzi wa mradi huo bila kujali kuwa walikuwa wanafanya kazi bila kula.

Alisema kilichobaki kwa sasa ni wananchi wa eneo hilo kuhamasishana, kuwapeleka watoto wao shule ili waweze kupata elimu ambayo ni urithi na ukombozi wa kifikra kwa jamii kwa ujumla.

Kuhusu ujenzi huo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Chingulungulu, Rajabu Yasini, alisema mradi huo serikali kupitia TASAF ilitoa zaidi ya Sh. millioni 77.796 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu, kwamba kwa sasa ujenzi wake umefikia asilimia 95.

Alisema hatua iliyobaki kwa sasa ni hatua za mwisho za kupiga rangi na kubandika malumalu ili wananfunzi waanze kusoma.

Diwani wa Muhuwesi, Imani Ngonyani, aliupongeza uongozi wa TASAF, halmashauri na serikali kwa kuwapatia msaada huo, akisema uchakavu na upungufu wa madarasa ni mkubwa katika maeneo yote ya Tunduru.

Alisema yeye na wananchi wamejipanga kufanya kazi kwa kujitoa katika miradi mingine itayohitajika katika eneo hilo ikiwemo ujenzi wa zahanati.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Tunduru, Muhidini Shaibu, alisema katika utekelezaji wa mradi wa kunusuru kaya masikini serikali ilipeleka mradi wa ujendi ujenzi wa madarasa matatu yenye thamani ya Sh. milioni 77.7 baada ya kubaini uwepo wa uhitaji mkubwa katika kijiji hicho.

Alisema mradi huo unaendelea vizuri na kilichobaki kwa sasa ni TASAF kukamilisha taratibu za kununua malumalu ili wanafunzi waanze kusoma.

# Shule 3,000 kuunganishwa mafunzo kidijitali

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa kushirikiana na kampuni ya simu za mkononi ya Airtel, limezindua mradi uitwao 'Smart-Wasomi' ambao utaunganisha shule za sekondari 3,000 na mtandao.

Lengo ni kuwezesha upatikanaji wa maudhui ya kujifunza kidijitali kutoka maktaba mtandao ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo juzi jijini Tanga, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema uwiano wa sasa wa vitabu kwa mwanafunzi katika shule nyingi za umma haukidhi viwango vilivyowekwa na serikali,

"Kujifunza kidijitali ndiyo njia ya haraka zaidi ya kuboresha matokeo ya kujifunza na kuandaa watoto wetu kwa ajili ya siku zijazo.

Kwa hiyo serikali inaipongeza Airtel na UNICEF kwa kuendeleza mpango huu ambao unasaidia juhudi za serikali zinazolenga kuongeza upatikanaji wa elimu ya kidijitali kwa watoto wetu," alisema Majaliwa.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, alieleza kuwa mradi huo siyo tu utapunguza mgawanyiko wa kidijitali bali pia utafungua na kuongezea tija wanafunzi katika kuendelea kujifunza kupitia mtandao ambao utatoa huduma hiyo bure kwao kupitia maudhui ya kidijitali kutoka maktaba mtandao ya TEA.

"Mpango huu utasaidia kuongeza viwango vya ufaulu na ubora wa elimu kwani bila shaka utaimarisha vijana wetu kustawi kuwa na uzoefu zaidi katika ulimwengu huu wa kidijitali.

Tunajivunia kuunga mkono jitihada hii na tunatazamia kushuhudia matokeo chanya katika elimu nchini Tanzania," alisema Profesa Mkenda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Tanzania, Dinesh Balsingh, alisema walianza utekelezaji wa dhamira ya kusaidia elimu kidijitali mwaka 2015 kwa kuzinduzia mradi wa VSOMO kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Alisema Airtel imekuwa na ushirikiano na Dar Teknohama Business Incubator (DTBi) kwa kuzindua maabara ya kidijitali inayowajengea vijana na wajasiriamali uwezo wa TEHAMA ili waweze kusimamia biashara zao kwa ufanisi zaidi.

Mwakilishi Mkazi wa UNICEF, Elke Wisch, alisema takwimu zinaonyesha kuwa mamilioni ya watoto Afrika wanapata changamoto katika kupata nyenzo bora za kujifunzia kutokana na rasilimali chache.

Mradi huo utaendeshwa kwa miaka mitano, umekuwa na mafanikio katika awamu ya kwanza ya majaribio ambako tayari shule za sekondari 50 katika mikoa ya Dodoma, Mbeya na Zanzibar zimeshaunganishwa.

Pia, zaidi ya walimu 2,000 wameshapatiwa mafunzo, huku wanafunzi 55,000 wameshafikiwa na wanaendelea na mafunzo.




Mkurugenzi wa Maendeleo na Matumizi ya Kiswahili kutoka Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Kulwa Kindija (kushoto), akizungumza katika uzinduzi wa Chama cha Sarufi ya Kiswahili Tanzania (CHASAKITA), mjini Bagamoyo, mkoani Pwani juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Elimu ya fedha yawafikia walimu

**Na Mwandishi Wetu,**
BIHARAMULO

TIMU ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha inayotoa huduma ya elimu ya huduma ndogo za fedha ,imewafikia walimu wa shule za msingi, sekondari na wakuu wa idara za elimu na kuwaelimisha kuhusu masuala ya fedha ikiwamo kujiepusha na mikopo isiyo salama, maarufu kama kausha damu

Semina hiyo ilifanyika juzi katika ukumbi wa St. Clara, wilayani hapa na zaidi ya walimu 650 walishiriki na kupata fursa ya kujifunza mada nne zikiwamo kujiwekea akiba, mikopo, uwekezaji, na usimamizi wa fedha binafsi.

Mmoja wa washiriki, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mizani, Ephransia Zakayo, alisema kuwa kupitia semina hiyo amejifunza kuwa kabla ya kuchukua mkopo ni lazima kuainisha malengo ya kufanya hivyo lakini pia matumizi ya mkopo na namna ya kupanga kurejesha ili kutokuingia kwenye migogoro.

"Kupitia elimu hii nimejifunza pia umuhimu wa kuwa na vipaumbele katika maisha yetu ya kawaida. Ukiwa na vipaumbele, itakusaidia kutokuwa na tamaa na itasaidia kutokukupeleka kwenye mikopo ambayo hukupanga kuchukua", alisema Zakayo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kikomakoma, Lukanga Yassin, aliishukuru serikali kwa kuwafikia na kuwapa elimu ambayo imewapa uelewa mpana wa masuala ya fedha ikiwamo kuwa na matumizi sahihi na kuweka akiba wanapopata fedha badala ya kuzitumia zote.

Naye Afisa Usimamizi wa Fedha Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha Wizara ya Fedha, Stanley Kibakaya, alisema kumekuwa na mwitikio mkubwa kwa walimu na wameonyesha nia ya kufanya uwekezaji katika taasisi mbalimbali rasmi.

"Katika makundi mbalimbali tuliyowafikia, wananchi wameahidi kubadilisha mtindo wa maisha ikiwamo kuacha kukopa kwa mazoea lakini pia kuanza utaratibu wa kusoma mikataba kabla ya kusaini ili kupunguza kama sio kumaliza kabisa migogoro ya mikopo" alisema Kibakaya.

Kwa kutambua umuhimu wa elimu ndogo ya fedha kwa wananchi wa Tanzania mwaka 2021, serikali kupitia Wizara ya Fedha ilianzisha rasmi Wiki ya Huduma Ndogo za Fedha ambayo hufanyika kila mwaka, ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kila mwananchi anafikiwa na elimu ya huduma ndogo za fedha katika ngazi zote za mjini na vijijini.

Kwa sasa, timu ya wataalam hao kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na taasisi zingine za serikali, imemaliza utoaji elimu ya huduma ndogo za fedha kwa wananchi wa mikoa ya Kagera, Singida na Manyara.

Timu hiyo sasa inakwenda katika mikoa ya Rukwa na Kigoma kuwafikia wananchi na kupatiwa elimu ya huduma ndogo za fedha ili kuwa na uelewa mpana wa masuala ya fedha ikiwa ni utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kwa mwaka 2021/2022 hadi 2029/2030.

JUNI 2, 2024
Nipashe

# MAISHA

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 13

**MITINDO UFUKWENI**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Sakafu bora zina mchango kupendezesha nyumba



Ukurasa 12





# ASALI NA MDALASINI

## Inavyokupa mwonekano kamili

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | | S | W | A | L | A |
| H | | | | G | | S |
| A | | B | U | U | | T |
| W | A | O | | S | A | A |
| A | | N | A | E | | A |
| B | | D | | | | F |
| U | J | A | Z | O | | U |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

JII, MIA, KOO, MEI, SHIMO, APONE, JIMBO, ITIKA, ONGOZWA, CHIMBWA

## TOA TOFAUTI 5





## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

NI WAKATI WA KUREJEA NYUMBANI






MTOTO Suzana akiwa varandani na mama yake akimsaidia kazi za nyumbani. Wakati wakiendelea na kazi Suzana alimuuliza mama yake.

**Suzana:** Mama naomba nikuulize kitu kuhusu bahari

**Mama Suzana:** Sawa niulize tu

**Suzana:** Eti kuna samaki anayeitwa Nguva anafanana na binadamu, tena mrembo kama malaika?

**Mama Suzana:** Hakuna samaki wa aina hiyo

**Suzana:** Kumbe wanatuongopea hakuna samaki Nguva?

**Mama Suzana**: Samaki Nguva yupo lakini hana umbo la binadamu, hayo ni mapokeo na hadithi tu.

============

**SWALI**

Swali; Paa ni jamii ya Mnyama gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Dalili ndoa inafuatiliwa na nguvu za giza

KARIBU msomaji wangu tuendelee na uchambuzi wetu kuhusu purukshani ndani ya ndoa zetu. Wiki iliyopita nilijadili roho kuu zinazoangamiza ndoa. Nikataja roho za kichawi, roho za mizimu na roho za majini mahaba.

Leo twende zaidi tuone dalili zinazoonyesha kuwa ndoa yako inafuatiliwa na nguvu za giza. Kabla sijazitaja, nirudie kusema kwamba tatizo kubwa ambalo mwanadamu anaweza kupitia katika maisha yake ni tatizo la ndoa.

Ni rahisi kukabiliana na changamoto za biashara lakini siyo rahisi kukabiliana na mafarakano katika ndoa. Kadhalika nimegundua kuwa matatizo makubwa katika ndoa za watu wengi, yana chimbuko refu sana la kishetani.

Wengi wanaopitia matatizo makubwa sana ya ndoa hawajui kuwa nguvu za giza zimeachiliwa kuua hatma za maisha yao. Nguvu za giza zinashambulia ndoa zao kama njia mojawapo ya kuua hatma zao!

Wako mawakala wa shetani ambao wameachiliwa kufuatilia mtu yoyote anayelalamika kuwa ana mafarakano katika ndoa ili wamuangamize kabisa.

Hebu sasa msomaji wangu nikipitishe kwenye dalili kuwa ndoa yako inafuatiliwa na nguvu za giza. Kwanza ni mafarakano ya ndoa yasiyoisha.

Kwenye safari ya ndoa huwa kuna nyakati wanandoa wanatofautiana. Na tofauti hizi husababisha migongano na mafarakano; na baada ya kusuluhishana, maisha huendelea kama kawaida. Ukiona kwenye ndoa yako kuna mafarakano yasiyoisha, tafuta msaada!

Dalili nyingine ni kuchukia ndoa. Pale unapokuwa kwenye ndoa lakini unatamani tu uachike hata kama hakuna mafarakano kwenye ndoa yako, ujue unahitaji msaada.

Nyingine ni pale unapoota unazini na wanadamu au viumbe kwenye ndoto. Kumwadhibu mwenzi wako kwa kutoka nje ya ndoa kama kumkomoa. Kuota una mimba kwenye ndoto. Kuota unanyonyesha kwenye ndoto. Kuota umelala na mwanamke aumwanamume pembeni yako.

Dalili nyingine kuota una familia nyingine kwenye ndoa. Kuota unahemea vitu na mwanaume aumwanamke sokoni au kwenye maduka makubwa. Matatizo ya uzazi. Pale unapoharibu mimba baada ya kuota ukizini na mwanaume kwenye ndoto. Kuota unafunga ndoa kwenye ndoto. Kujutia ndoa yako kila mara. Kukosa uaminifu kwa mkeo aumumeo. Unaota kuwa wewe ni tajiri na una fedha nyingi wakati wewe ni masikini katika uhalisia.

Unaota unacheza na nyoka. Kumchukia mumeo au mke wako bila sababu yoyote. Kuota unaogelea kwenye mto, ziwa au baharini. Magonjwa ya ngozi yanayosababisha mwili kuwasha na hata ukitibu hayaponi.

Pia umasikini uliokithiri. Kifo cha ghafla cha mwenzi wako. Kupoteza kazi mara baada ya kufunga ndoa. Majanga kama moto kuunguza nyumba, ajali ya gari, kufungwa gerezani mara baada ya kufunga ndoa. Kusikia sauti zikikwambia ikimbie ndoa yako.

Kutelekezwa na mwenzi wako. Kupoteza pete ya ndoa mazingira tatanishi. Maumivu makali ya kiuno na mwili wakati wa hedhi. Kufanya kazi mbali na familia yako kunakowatenganisha kama mke na mume.

Hasira kali kwa mke au mume, kuchanganyikiwa, kupoteza nguo za ndani (gagulo au kiwalo), sidiria. Pale wakwe wanapotawala ndoa yako badala ya ninyi kutawala ndoa yenu.

Pale unapoanza kuhisi uzito wa kuwasiliana na mke au mume wako. Ukiona kuwa zamani ulikuwa na tabia ya kuwasiliana mara kwa mara na mke na mume wako ama kwa simu au mume akifika nyumbani unakuwa na shauku ya kuongea naye, iwe ni kupiga hadithi, kucheka pamoja na sasa unaanza kuhisi hofu kila unapomuona mwenzio, jua ya kuwa ndoa yako iko hatarini.

Tafuta msaada kwani leo wapo washauri wa ndoa wasomi. Pia wako watumishi wa Mungu wenye ndoa zenye mfano wa kuigwa waokoe hilo jahazi lenu kabla halijazama.

Msomaji wangu, dalili hizi na nyingine ambazo nitamalizia wiki ijayo, zimebomoa ndoa nyingi na zingine zinachungulia kufa huku wahusika hawajui chanzo halisi ni kipi.

Shetani na mawakala wake wamekulenga ili kukuangamiza ndiyo maana nataka uwe na hasira na shetani. Unatakiwa ufikie mahali uchukue maamuzi ya kumwambia shetani kuwa "sasa yatosha!"

Nafahamu ya kuwa kuna watu ambao hupambana na vitu kila wanapolala usiku. Wengi hawatulii kwa sababu wanahisi adui anawashambulia kila usiku.

Kwa nini ukubali maisha yako yawe uwanja wa vita wakati Mungu anakuwazia mema na siyo mabaya? Anasema "Njoo kwangu wenye mizigo nami nitawapumzisha...

**Dalili zaidi wiki ijayo. Maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Godfrey Mushi



# TGNP NA PELUM TZ, vita vyenu vina macho

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umeanzisha kile kinachoitwa kampeni maalum ya kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia, hasa ukatili wa kingono, mwanamke na uongozi na kilimo ikolojia.

TGNP inatekeleza mradi wa wanawake vijijini waletao mabadiliko (RWCC) na moja ya malengo mahsusi, ni kuongeza uelewa wa wanajamii katika kuchagiza mila na desturi chanya na kuondokana na mila kandamizi.

Wakati anafingua mafunzo ya siku tatu ya waandishi wa habari 24 kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Morogoro, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alinukuliwa akisema mtandao huo unalenga kupambana na ukatili wa kijinsia na kuhamasisha mabadiliko ya kimfumo na kitamaduni.

Vilevile, TGNP inalenga kuchagiza na kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi katika uchaguzi wa serikali za vijiji, mitaa na vitongoji utakaofanyika baadae mwaka huu.

Eneo lingine ni la kilimo ikolojia ambalo linahitaji msukumo wa wadau mbalimbali vikiwamo vyombo vya habari na wakulima, hasa kuhamasisha wanawake zaidi kushiriki katika kilimo hicho pamoja na kukipa uzito katika jamii.

Akizungumzia kuhusu kilimo ikolojia, Liundi amenukuliwa akisema kilimo hicho kina tija kubwa, licha ya kuwa ni cha asilia kwa sababu hakitumii dawa za kemikali.

Amesema kuwa serikali ya Tanzania inatambua kwa kiwango fulani kuhusu kilimo hicho na kuna juhudi ambazo zimekuwa zikifanyika.

Akitolea mfano amesema aerikali imeanzisha idara ya kilimo ikolojia katika Wizara ya Kilimo, ambapo kuna dawati mahsusi kwa ajili ya kuhamasisha kilimo hicho.

Katika mradi wa Wanawake wa Vijijini wa Kuleta Mabadiliko (RWCC), TGNP inashirikiana na Shirika la Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi Tanzania (PELUM Tz). Lengo la mradi huo ni kuwafikia wakulima wanawake 5,364.

Mradi huo wa miaka sita (2021/26), unatekelezwa katika mikoa wa Kilimanjaro, Manyara na Morogoro.

Tangu serikali iliposhtuka usingizini kuhusu kashfa ya ulawiti shuleni, kumekuwa na hekaheka nyingi za viongozi wa serikali, kupishana huku na huko wakikemea uchafu huo na wengine wakiweka hadharani misimamo yao.

Sakata la madai ya ulawiti na matukio mengine ya ukatili wa kingono, limeenda mbali zaidi katika mikoa hiyo mitatu.

Tunasahau kwamba, wazazi na walezi, wanapaswa kutafakari juu ya kupunguza harakati za kutafuta maisha, badala yake wawafuatilie watoto wao kuhusu dalili za ulawiti na ukatili mwingine dhidi ya watoto.

Ninavyoitazama mradi huu wa TGNP na PELUM Tz, natamani kama walimu wakuu wa shule za msingi na na wakuu wa shule za sekondari, wangeanzisha vitengo vya intelijensia ya wanafunzi shuleni pamoja na madawati ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto ili kupambana na tishio la ukatili wa kijinsia na vita dhidi ya ulawiti.

Inapendeza kwa ujio huo wa mbinu mpya za kukabili ulawiti, ubakaji na ukatili mwingine wa kingono dhidi ya wanawake na watoto.

Natamani Jeshi la Polisi kupitia Kitengo cha Polisi cha Ushirikishwaji Jamii na Dawati la Jinsia, wangeingia kazini kuwapika wanafunzi watakaoteuliwa kwa siri na walimu wao kuwa kikosi kazi cha intelijensia shuleni na ulinzi wao mitaani.

Nendeni mkawapige msasa kwa kuwapatia mafunzo maalum ya namna ya kufuatilia nyendo za wenzao shuleni, mitaani au majumbani; na namna ya kuwaripoti kwa usiri kwa 'mwalimu' ambaye atakuwa ameteuliwa kusimamia jukumu hilo ili kugundua mienendo ya wanafunzi na walimu wao.

Kwa kuwa intelijensia inahusika zaidi na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa mbalimbali za intelijensia, vikosi kazi vya wanafunzi vinavyounda intelijensia shuleni, ni vyema vikafundwa kuhusu usiri na namna ya kujiheshimu.

Aidha, uwekwe utaratibu kwa wanaoteuliwa kufanya kazi hiyo wasijuane, na wafundwe namna ya kufanya thathimini ya taarifa za kiintelijensia zinazohusu uadilifu wa wenzao, wakiongozwa na mwalimu maalum anayepokea taarifa hizo.

Mwalimu huyo maalum afundwe pia namna ya kuzichakata taarifa hizo, kabla ya kuwasilisha ripoti yake kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi au Mkuu wa Shule ya Sekondari ili kuchukua hatua.

Hatua si kufukuza shule kwa haraka, si kupiga, si kudhalilisha. Ni kukaa na mwanafunzi anayeonekana kutumbukia katika uchafu huo na kumdodosa alikopata mafunzo, alikoshawishika na nani alimfanyia ukatili huo ili kupata uhalali sasa wa kumuondoa kwa manufaa ya wengi au kumnusuru anayeonekana kuathiriwa na hali hiyo.

Wala sijakosea, tuvute subira!

*• Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com au simu ya mkononi: +255 767 535490*



KUMBUKUMBU NZURI KWA RAMADHAN MASHKANDO BAADA YA KUTIMIZA MIAKA MIWILI TANGU AFUNGE NDOA NA MKEWE KIPENZI. MUNGU AWABARIKI KATIKA MAISHA YENU YA NDOA.







MITINDO

Na Moshi Lusonzo

# MITINDO UFUKWENI kunogesha maharusi

NGUO za harusi kwa kawaida inawapa kwa maharusi wengi, wengi wanajikuta wanashindwa kununua nguo zinazoendana na tukio halisi.

Wataalamu wa masuala ya mavazi, wanasema idadi kubwa ya wanaooana wana ugumu wa kufahamu nguo zipi wanahitaji kwenda nazo kulingana na mahali na muda husika.

Kitu cha muhimu hapa ni kufahamu kuna tofauti ya gauni la ukumbini, kanisani na hata kwenda ufukweni.

Gauni la ufukweni, linatengenezwa maalum kulingana na hali ya hewa na mazingira halisi.

Kwa wale wanaotaka kuwa na gauni hilo kwa ajili ya kwenda ufukweni na kupiga picha za kumbukumbu, basi utakiwa kufuata mambo yafuatayo.

Kulingana na mahitaji ya mtu husika, kuna aina nyingi ya magauni ya ufukweni.

Jambo la kuzingatia unashauriwa kuvaa gauni lenye kitambaa laini ili kuendana na hali ya upepo.

Magauani yanayopendekezwa sana ni rangi nyeupe kwa sababu yanaakisi maji ya bahari .

Hata hivyo rangi yoyote inayopendekezwa na wahusika ni nzuri, isipokuwa bluu bahari.

Hakikisha mtu aliyebuni gauni lako anaweka vionjo tofauti na magauni mengine ambayo yametumika matukio ya nyuma.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# ASALI NA MDALASINI

## Inavyokupa mwonekano kamili

VIPELE aina ya chunusi vikiwa usoni, kifuani, mgongoni au sehemu nyingine yoyote ya mwili vinaweza kutoweka bila kutumia vipodozi vya kemikali.

Siyo mafuta pekee yanayoweza kutibu chunusi, bali 'scrub' zinazohusisha vitu vya asili ambavyo ni rahisi kupatikana.

Leo tutaelekezana namna ya kutumia mchanganyiko wa asali na mdalasini katika kumaliza tatizo la chunusi mwilini.

**Jinsi ya kutumia**

Chukua vijiko vitatu vya asali, nusu kijiko cha unga safi wa mdalasini na changanya pamoja kupata uji mzito kiasi.

Paka sehemu yenye chunusi na kisha kaa kwa angalau dakika 10 hadi 30, halafu osha kwa maji ya uvuguvugu.

Mdalasini unaweza kuwasha kwenye ngozi hivyo unashauriwa kujaribu kupaka kidogo kwenye kiganja cha mkono kwanza ili kupata uhakika kua haitakusumbua.

Endelea kutumia kwa wiki mara mbili mpaka utakapoanza kuona matokeo na kuendelea mara moja kwa wiki na hadi mara moja baada ya wiki mbili.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya tikiti maji na limao

NI nadra sana kukuta mtu anatengeneza juisi ya limao na tikiti maji, lakini mchanganyiko huu ni mzuri na wenye siri kubwa kiafya.

Leo utajua namna ya kutengeneza kinywaji hiki ambacho kitakufaa wakati wa mlo wako wa asubuhi, mchana au usiku.

**Mahitaji**

Tikiti maji la kilo tano, juisi ya limao gram 180, asali mbichi gramu 80, fungu moja la majani ya mint na vipande vya barafu

**Jinsi ya kutengeneza**

Katakata tikiti maji katika vipande vidogo, menya maganda na kumbuka kutoa mbegu.

Chukua vipande vya tikiti maji saga pamoja na juice ya limao.

Kisha ichuje katika chujio safi baada ya kuisaga.

Kisha weka barafu pamoja na majani ya mint katika jagi.

Halafu mimina juisi katika jagi lako lenye barafu na majani ya mint.

Mimina asali mbichi kwenye mchanganyiko wa juisi na ukoroge ichanganyike.





## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Sakafu bora zina mchango kupendezesha nyumba

KILA uchao tunashuhudia mabadiliko yanayojitokeza maishani ambayo kwa namna mbalimbali yanasababishwa na maisha ya utandawazi tuliyo nayo katika karne ya leo.

Mambo yaliyofanyika jana si yale yanayofanyika leo na si yatakayofanyika kesho wala keshokutwa. Kila siku yanaibuliwa mapya ama kwa mtindo mwingine au kwa ubora zaidi endapo yaliwahi kufanywa.

Leo tunaangalia ubora uliopo sasa katika uwekaji wa sakafu ndani ya nyumba. Katika nyumba, sakafu ni miongoni mwa vitu vinavyochangia kupendezesha nyumba na hata pale inaposakafiwa kwa utaalamu mzuri.

Yako baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kusakafia nyumba ambayo Msanifu Majengo, David Kashozi, anayaeleza kuwa kabla ya kuweka sakafu ni muhimu kuangalia rangi ya nyumba ili visipishane sana.

Jambo la pili ambalo anasema linapaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi wa sakafu ni ubora wake na jambo la tatu ni kuchagua sakafu ambayo ni rafiki na salama kwa makundi yote ya watu wanaoishi katika nyumba yako.

"Chagua sakafu ambayo haitawakwaza baadhi ya watu kulingana na umri wao hususani watoto, wazee na wagonjwa maana zingine zina utelezi mkali," anasema Kashozi.

Jambo la nne, kwa mujibu wa Kashozi, ni vizuri kuzingatia kuchagua sakafu ambayo ni bora na inadumu kulingana na bajeti uliyojiwekea kabla ya kubadili nyingine.

"Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora lakini inaendana na wakati," anasema Kashozi.

Mtaalamu hiyo anamalizia kwa kushauri jambo la tano kwamba ni vyema kufanya maandalizi mapema ya aina ya sakafu unayoitaka.



## DONDOO

**Na Restuta James**

### Tengeneza mazingira kujisomea nyumbani



FAMILIA nyingi kama sio zote zenye uwezo wa kununua televisheni au radio wanazo. Nyumba hizo hizo, ni chache au chini ya nusu hazina maktaba walau ya vitabu vichache.

Hali hii imejenga tabia ya wanafamilia na hasa watoto kupenda kuangalia na kusikiliza vipindi zaidi badala ya kusoma.

Kama wewe ni mzazi au mlezi nakuletea mbinu ya kuanzisha maktaba ndogo nyumbani ili watoto wanufaike na maarifa mengi yaliyofichwa vitabuni.


Walimu wa watoto wadogo wanaeleza kuwa mtoto mwenye umri kuanzia miaka miwili na nusu wanauwezo wa kujifunza kusoma na wakajua ndani ya muda mfupi, kama mazingira wenzeshi wataanzia nyumbani.

Wanashauri kuwa ni wajibu wa mzazi/mlezi kujenga tabia ya kujisomea nyumbani.

- Tengeneza shelvu la kuvutia
- Tenga muda wa kusoma pamoja
- Mpe mtoto muda wa kuzijua herufi, anaposhindwa kwenda kwa kasi unayoitaka usimwadhibu
- Usisome tu, chora pia

Kwa wenye nyumba kubwa, tenga chumba kikubwa kwa ajili ya maktaba, kwa wenye nyumba ndogo tengeneza shelvu za ukutani kama zinavyoonekana pichani au kwa jinsi utakavyoona inafaa.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
HUYO NDIO MUME WANGU SIMAMA UONGEE NAE NAMJUA MTAELEWANA TU!
ANAMILIKI 'BUCHA' YULE!
UCHAGUZI UJAO MAONI YAKO 'NITATOBOWA?'
KWANZA NAMBIE KAMA HUJATEMBEA NA BASTOLA KABLA SIJAKUJIBU
NIMEFANYA UGONI LAKINI LEO NIMEFIKA KWENYEWE!
EEEEH?
UMEVULIA SHATI MSOSI USIOUJUA UMEPATIKAJE!
NIKISHIBA NIANDALIE MAELEZO.
MBONA SIKU HIZI SIKUSIKII TENA UKINIPIGIA SIMU NA KUNIULIZA NATAKA NINI?
'NIMEKOMA!'
SWALI LA KISAYANSI UKITAKA KUFUNGA KAMBA ZA VIATU NINI KINATOKEA?
SOGEA KARIBU NIKUJIBU!
FISADI

HABARI KIMATAIFA

# Serikali ya mseto yanukia Afrika Kusini

**PRETORIA**, AFRIKA KUSINI

KULINGANA na matokeo ya uchaguzi wa Afrika Kusini yanayoendelea kutoka, Chama cha Africans National Congress (ANC) kimezidi kupoteza viti vya wabunge na kusababisha uwezekano wa kuundwa kwa serikali ya mseto nchini humo.

ANC ambayo imetawala nchi hiyo kwa miaka 30, tangu kumalizika kwa utawala wa kibaguzi, itakuwa na chaguo la chama gani kinaweza kushirikiana ili kuunda serikali hiyo ambayo itakuwa ya kwanza katika historia ya nchi hiyo. Katika matokeo yaliyotangazwa hadi jana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (IEC), asilimia 80 ya kura zimekwisha kuhesabiwa, chama tawala cha ANC kimepata asilimia 40 ya kura zote za wabunge.

Chama kikuu cha upinzani cha Democratic Alliance (DA) kinachoongozwa na John Steenhuisen, kimefanikiwa kupata asilimia 22.16% ya kura huku chama kilichoanzishwa miezi sita iliyopita na rais wa zamani Jacob Zuma, UMkhonto Wesizwe (MK), kikijipatia asilimia 13.06.

Hata hivyo, chama cha wapiganaji ukombozi wa kiuchumi, (EFF), cha Julius Malema kimefikisha asilimia 9.41 ya kura zote.

Ikiwa hadi matokeo ya mwisho ambayo yatatangazwa leo yatabaki kama ilivyo, chama hicho kinachoongozwa na Rais Cyril Ramaphosa, hakitakuwa na njia mbadala bali kukubali kuingia katika muungano wa vyama.

Katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, tangu kuanza kwa demokrasia nchini humo mnamo mwaka 1994, ANC imekuwa ikishinda chaguzi kwa wingi wa kura na kuongoza taifa hilo lililoimarika zaidi kiuchumi barani Afrika bila muungano. Kulingana na matokeo ya awali, ANC pia itapoteza wingi wa kura katika jimbo lililoimarika kiuchumi la Gauteng, ambao unapatikana mji mkuu Pretoria na kitovu cha biashara jiji la Johannesburg. Chama hicho kimepata kura ya chini ya asilimia 50 katika eneo la KwaZulu-Natal, ambako ni nyumbani kwa Zuma.

Jimbo la Cape Magharibi, ambalo ni la pili kwa nguvu ya kiuchumi limetawaliwa kwa miaka mingi na chama cha DA na matokeo ya awali yanaashiria kuwa chama hicho kitahifadhi wingi wake wa kura katika eneo hilo.Baada ya kutangazwa matokeo ya mwisho, bunge jipya litakalochaguliwa litatakiwa kuunda serikali na kumchagua rais ndani ya siku 14.

Taifa hilo lenye idadi ya watu milioni 61, linakabiliwa na uchumi mbaya pamoja na kiwango kikubwa cha ukosefu ajira .

Pia taifa hilo linakabiliwa na ukatikaji wa umeme mara kwa mara pamoja na viwango vya juu vya uhalifu na rushwa.

**DW**



Raia wa Palestina wakiangalia masalia baada ya shambulizi lililofanywa na vikosi vya Israel katika mji wa Rafah jana. **PICHA: ALLIANCE**

# Israel yazidi kuiangamiza Rafah

**GAZA,** PALESTINA

VIKOSI vya jeshi la Israel vimeendelea kuushambulia mji wa kusini mwa Gaza wa Rafah, wakati Rais Joe Biden wa Marekani akitangaza kwamba nchi hiyo imetoa mwelekeo mpya wa usitishwaji kamili wa mapigano.

Muda mfupi baada ya tangazo hilo la kiongozi huyo wa Marekani, Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alitoa ujumbe na kusisitiza kwamba nchi yake, itaendelea na vita hadi itimize malengo yake yote, ikiwemo kulitokomeza kundi la Hamas.

Chini ya mpango huo uliowasilishwa na Biden na ambao kundi la Hamas limesema linautafakari, Israel imependekeza hatua tatu muhimu za kumaliza vita.

Hatua ya kwanza itakuwa ni kipindi cha wiki sita cha usitishaji mapigano ambacho kitashuhudia vikosi vya Israel vikiondoka kwenye miji yote iliyo na watu wengi katika Ukanda wa Gaza.

Kisha itafuatiwa na hatua ya pili na ya tatu inayojumuisha kubadilishana mateka wote na wafungwa, na baadae vikosi vya Israel vitaondoka katika ardhi yote ya Gaza na baadaye utaanza mpango wa kuijenga upya Gaza.

**DW**

# Mapigano makali yaendelea Goma

**GOMA,** DRC

MAPIGANO makali yanaendelea kurindima mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kati ya jeshi la serikali na wakati wapiganaji wa M23.

Kulingana na Umoja wa Mataifa, kwenye mapigano hayo kundi la wanamgambo wanaojiita wazalendo wanaisaidia serikali wamejiunga katika mapambano hayo karibu na mji wa Goma.

Katika siku za hivi karibuni, mapigano yameongezeka, na kusababisha watu wengi kuhama makazi yao.

Juzi Ijumaa mapigano yalikuwa makali katika maeneo mawili ya Sake.

Mji wa Sake, ambao uko karibu kilomita 27 kutoka mji wa Goma ambao ni makao makuu ya jimbo la Kivu Kaskaziniuliendelea kukabiliwa na mashambuzlia kwa siku ya pili mfululizo na kusababisha watu kukimbiamakazi yao.

Wanajeshi wa serikali walisema wanajibu mashambulizi hato ya M23.

Wakati wa mapigano, wanajeshi wasiopungua 13 wa Afriak Kusini kutoka kikosi cha SADC walijeruhiwa na mmoja aliuawa.

Kulingana na ripoti za jeshi la Afrika Kusini, magari mawili ya kivita yaliharibiwa.

Katika moja ya barabara za mji huo, FARDC imekuwa ikifanya mashambulizi kwa siku kadhaa karibu na Bweremana, mji ulioko kilomita 50 kutoka Goma.

***RFI***

# Rais Ferdnand Marcos wa Ufilipino yaionya China

**MANILA,** UFILIPINO

RAIS wa Ufilipino Ferdinand Marcos Jr, ameionya nchi ya China kutovuka mstari mwekundu katika suala la Bahari ya China Kusini, ambako mataifa hayo mawili wangombania. Kiongozi huyo alisema iwapo raia yeyote wa Ufilipino atafariki kutokana na hatua za makusudi kutoka China, itachukuliwa sawa na kukaribia vita na nchi yake itajibu kwa ukali.

Rais Marcos alikuwa akizungumza katika kongamano la usalama nchini Singapore lililohudhuriwa na wakuu wa ulinzi kutoka sehemu mbalimbali duniani, ikiwemo Marekani na China.

Akijibu kauli hiyo, msemaji wa jeshi la China, aliishutumu Ufilipino kwa kuelekezea lawama nchi yake kwa kuishambulia kwa maneno. Katika miezi ya hivi karibuni mgogoro wa muda mrefu kati ya China na Ufilipino kuhusu eneo katika Bahari ya China Kusini umezidi kukua kwa kasi. Ufilipino imelalamika kuhusu meli za kushika doria kutoka China kurusha maji ya kuwasha kwenye boti za Ufilipino na meli za kusafirisha bidhaa nchini humo. Hata hivyo serikali ya China imeeleza inatetea uhuru wake.

***BBC***

MAKALA

# UNAWEZA KUWA NA HAKI, UKAKOSA UHALALI



Na Magabilo Masambu

**Ni kweli kwamba mzazi alikuwa na haki ya kuitwa kama mzazi lakini uhalali wa kuwa mzazi ambaye tungetegemea amrekebishe binti yake ulikosekana. Maana yake ni kwamba ikishakuwa hivyo mzazi anakosa uhalali wa kumkanya binti yake japo anayo haki ya kumlea kama mwanawe.**

KUNA wakati nafasi za madaraka au kisiasa huwafanya baadhi ya viongozi kudhani kwamba zinafuta upungufu au kasoro zao na kujiona wakati wote wako sahihi kufanya lolote. Wanadhani hivyo kwa sababu madaraka yanawapatia uhalali hata kama hawana haki hiyo ama kwa mujibu wa sheria au kwa utamaduni tu.

Kuna tofauti kubwa kati ya maneno haya mawili, haki na uhalali. Haki huwa inaonekana zaidi kuliko uhalali.

Unaweza kuwa na haki ya kutenda au kusema jambo fulani lakini ukakosa uhalali. Ikitokea ukatumia haki wakati unakosa uhalali, ukitenda jambo fulani wako watakaoona ni uonevu na mara nyingi huwezi kurekebisha tabia au kasoro kama utakuwa na haki lakini ukakosa uhalali.

Hali hii imewakuta watu wengi katika utendaji wao. Siku zote nafsi huwa inatukumbusha kabla ya kutenda lolote, inakuuliza je, unao uhalali wa kulisema au kulitenda hili? Wako wanaotenda mambo lakini baada ya kutenda, wakikaa wenyewe huwa bado nafsi inaendelea kuwakumbusha je, ni kweli ulikuwa na uhalali wa kulitenda?

Wako ambao wamewahi kuahirisha kusema au kutenda mambo fulani fulani kwa kuhukumiwa na nafsi kama wanao uhalali wa kuyatenda.

Siku moja nikiwa katika shule fulani, alipatikana mwanafunzi mmoja wa kike ambaye alivaa sketi fupi kiasi kwamba hakuwa anaweza hata kuokota kalamu chini iwapo ingedondoka.

Mwanafunzi yule ikabidi aitwe kwenye ofisi ya malezi, akapewa adhabu na akaagizwa akamwite mzazi wake. Binti yule akaenda nyumbani bahati nzuri, akamleta mama yake mzazi.

Walipofika shuleni kabla ya mazungumzo, yule mzazi alipewa kanga kwanza ili ajifunike, maana nguo aliyokuja nayo ilikuwa fupi kuliko ya mwanafunzi (mwanawe).

Ni kweli kwamba mzazi alikuwa na haki ya kuitwa kama mzazi lakini uhalali wa kuwa mzazi ambaye tungetegemea amrekebishe binti yake ulikosekana.

Maana yake ni kwamba ikishakuwa hivyo mzazi anakosa uhalali wa kumkanya binti yake japo anayo haki ya kumlea kama mwanawe.

Familia nyingi ambazo watoto wa kwanza walikataa shule ni mara chache sana kukuta watoto waliofuatia kuzaliwa wakiwa wamesoma. Sababu yake ni kwamba yule aliyetangulia kukataa kusoma anayo haki ya kuwaambia wadogo zake wasome lakini anakosa uhalali kwa sababu wanaweza kumwambia mbona hata wewe ulikataa shule? Utashindwa kujibu swali hilo na wakati mwingine unaweza kuwaona kama wanakudharau.

Daktari anayevuta sigara huku akisema kwamba sigara ina madhara, haki kama daktari mwelimishaji anayo, lakini anakosa uhalali. Elimu yake pia inakosa nguvu japo anayoyazungumza yana ukweli. Lakini ikiwa utapata ushauri kwa daktari ambaye havuti, ushauri huo utakuwa na nguvu zaidi na kuna uwezekano wa kuufanyia kazi.

Nimefanya utafiti kidogo hasa maeneo ya vijijini kwa sababu binafsi ni zao la kijijini, nimeishi huko nimeyaona hayo.

binti wa kwanza amepata ujauzito, mabinti wengine pia wamekuwa wakipata wngali wakiwa makwao na sababu yake ni kwamba yule dada mkubwa, anakosa uhalali wa kuwaambia kwamba si vizuri japo anayo haki kama dada mkubwa, hivyo hata wakifanya matendo hayo atabaki kuwatazama tu.

Akinyanyua mdomo tu, wanamwambia mbona na wewe ulifanya hivyo.

Vivyo hivyo ukiwa kiongozi mahala fulani ni lazima kuchunga matendo yako.

Kuna wakati unaweza kuwa na haki kabisa ya kuzungumza na mambo unayoyazungumza ni ya msingi, lakini ukakosa uhalali kwa wale wanaokusikiliza.

Si kwamba umeongea mabaya, watakuuliza mbona wewe ulifanya haya na yale? Ni jambo baya sana ukishakosa uhalali wakati ukiwa na haki kwa sababu mambo mengi itakubidi uwe unabaki nayo moyoni japo unajua yanakosewa.

Watu watakupinga si kwa sababu ya yale unayozungumza bali kwa sababu unakosa uhalali na kukosa uhalali huko kumesababishwa na matendo yako ya kila siku au ambayo umewahi kuyafanya huko nyuma.

Ukipewa nafasi ya madaraka ni muhimu kujua kwamba madaraka hayadumu, hivyo lazima uwe na tahadhari ya kesho itakuwaje. Usitende ukamaliza maana matendo hayo yatakuhukumu kesho na pengine milele.

Haki tulizo nazo kisiasa au kisheria zisitumike kudhalilisha utu wa watu wengine kwa sababu kesho watu wao waweza kuwa wakubwa kuliko sisi maana yuko mtu amewahi kusema uongozi ni koti la kuazima utavaa leo na utapendeza sana lakini wakati wowote mwenye nalo anaomba koti lake.

Tutende kwa busara kwa sababu twaweza kuwa na haki kisiasa lakini tukakosa uhalali kijamii.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Siri ni yako, yenu, akishiriki, kujua mwingine si siri tena*



Na Adam Fungamwango

**Kwa dunia ya sasa ya utandawazi, kuna siri za teknolojia, kila nchi ina wavumbuzi na wanasayansi wao ambao wanatengeneza au kuunda vitu vya kisasa, wanaficha wengine wasijue huwa anafanya nini, hiyo ni siri.**

SIRI ni nini? Kwanza tuanzie hapo. Ni taarifa, habari au matukio ambayo mtu fulani anayo au yamempata bila mtu yeyote kujua, ambayo inapaswa abaki nayo moyoni. Pia ni jambo lolote ambalo mtu analiona halifai kumshirikisha mtu yeyote yule, haijalishi ni nani. Vile vile ni uwezo wa kudhibiti mambo ambayo watu wengine hawayafahamu kuhusu wewe.

Inawezekana kuhusu mambo uliyoyafanya au unayofanya, kuficha taarifa zako nzuri au mbaya ambazo yoyote akifahamu inaweza kuleta matatizo, kukuvunjia heshima mbele ya jamii, au kuhatarisha maisha yako, au ndoa. Inawezekana ikawa ni nyaraka za benki, namba za simu za kuchukulia pesa, nyumba, mashamba, mahusiano, na vingine vinavyofanana na hivyo.

Kusema kweli, siri ina maana pana sana kwa sababu baadhi ya watu wanadai kuwa siri ni ya mtu mmoja tu na hakuna siri ya watu wawili.

Hapa kuna ufafanuzi kidogo. Kama nilivyosema neno siri ni pana sana, ni kweli kuna siri inayotakiwa uwe nayo wewe tu na si mtu mwingine.

Yeyote akijua basi itakuwa umejiweka matatani. Halafu kuna siri ya ndani, hii inahusu familia, hasa mke tu. Halafu ipo inayowashirikisha watoto, ambao pia kuna siri ambayo hawatakiwi kufahamu ya baba na mama yao.

Ukiacha hiyo kuna siri za ndugu, hasa wale waliozaliwa pamoja. Huwa wana siri zao ambazo ni wao tu wanatakiwa wazifahamu kama vile magonjwa ya kurithi na mengine yanayofanana na hayo.

Wakati mwingine yakiwekwa wazi na wapo kwenye jamii ya watu wachache, hasa vijijini wanashindwa kuoa au kuolewa, labda watoke na kwenda mbali.

Siri inakwenda mbali zaidi, kwani kuna ya kikundi fulani cha kijamii, kundi la wasanii, wanamuziki wa dansi, kijiji, na hata makampuni pia huwa na siri zao.

Huwezi kuchukua ya huku kupeleka huku, utaonekana msaliti na wakikubaini ni lazima wakuchukulie hatua.

Kama ulishawahi kusikia mawaziri wanaapa, kuna neno wanasema: "Sitotoa siri za Baraza la Mawaziri..." Hapa inaonyesha hata wao wana siri zao ambazo hazitakiwi kabisa kutoka nje kwa manufaa ya taifa.

Nchi nazo pia zina siri, ambazo zikijulikana kwa mataifa mengine ni hatari hata kama ni taifa rafiki kwani siku zote nchi zote duniani hazina urafiki wa kudumu, au uadui wa milele. Hivyo ni muhimu kuficha siri za nchi.

Wako pia watu maalum ambao ikibainika kuna mtu ameingia na amechota mambo fulani ambayo ni siri, wanashughulika naye. Mataifa yote duniani yapo hivyo.

Kwa hiyo siri inaanzia ya kwako mwenyewe, hadi ile ya nchi. Kama una mchepuko sehemu, hii inakuwa ni siri yako mwenyewe, mkeo huwezi kabisa kumwambia.

Kwa dunia ya sasa ya utandawazi, kuna siri za teknolojia, kila nchi ina wavumbuzi na wanasayansi wao ambao wanatengeneza au kuunda vitu vya kisasa, wanaficha wengine wasijue huwa anafanya nini, hiyo ni siri.

Wanamuziki wetu nao wanasemaje kuhusu siri? Muziki wa dansi haukuacha kitu. Umezungumzia pia mambo hayo.

Bima Lee, miaka ya 1980, walirekodi kibao walichokiita, 'Siri Yako.' Kina mashairi yanayosomeka hivi;

"Kitendo unachofanya umefanya nisikuthamini nikuelewe vibaya eee, ni mengi unayotenda moyoni unajidanyanya kama unafanya siri eee.

Siku nyingi nilisikia, watu wengi wakizisimulia habari zako wewe, mitaani zimeenea.

Siri yako ni yako eee, siri yako ni yakoo ee, akishiriki mwingine si siri tena.

Wengi hujidanganya kwa kufanya siri, huku akinena utadhani kasuku, watu huzipta wakazisambaza, nao wakijua hubaki kuduwaa, siri eee, siri, si siri tena.

Siri yako ni yako eee, siri yako ni yakoo ee, akishiriki mwingine si siri tena."

Maudhui ya wimbo huu ni kwamba jamaa ana mambo yake ambayo kwake ni siri. Lakini 'friji lake haligandishi'. Anapita anazungumza huku na huko, kwa hiyo badala ya kuwa siri, inageuka kuwa taarifa.

Bendi ya Orchestra Safari Sound, iliyokuwa inatumia mtindo wa Masantula Ngoma ya Mpwita, chini ya uongozi wa Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki', miaka hiyo hiyo ya mwanzoni mwa 1980, ilirekodi kibao kilichoitwa pia, 'Siri Yako.'

"Siri yako ni siri yako, siri yako weka moyoni, ukorofi, ugomvi, starehe ndani na mama watoto usitangazie mitaani, usisemeseme kama chiriku mwishoni utasema uongo, heshima yako yote itavunjika mbele wenzako na watoto.

Nilipolala, nilipoamka, nilipolala nipoamka,nilichokula jana na leo wameshatangazia, ni aibu kubwa hiyo usitangaze maisha ya wenzako." Hii ndiyo maana pana ya neno siri.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-10

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MFANO tu nitakutajia wachache, kuna Subiyani. Hili kazi yake ni kusababisha ajali na kunyonya damu za watu. Sehemu ambazo linapenda kukaa ndiyo zile ambazo ajali kutokea mara kwa mara. Kuna Makata, hiki linasababisha vifo kwa watu mbalimbali na binadamu hulitumia kwa kulipiza kisasi kwa alichotendewa na mhusika." Mzee Raia alimwambia Heri ambaye aliendelea kushangaa kwa kile anachoambiwa.

"Kuna lingine linaitwa Subha, hili jini likimpata au kumwingia mtu linasababisha kuwa na kiburi sana na kujikweza. Maulan, likiwaingia watu linawafanya kuwa vichaa, Abuni, linamfanya mtu kuwa na hasira, Al Tarik lenyewe linapoteza watu katika mazingira ya kutatanisha,

Zaitun, lenyewe linasababisha wasichana kuwa na maringo, na Shamsu hili huvaa umbile la binadamu kwa sura yoyote na majini haya ndiyo yale ambayo huwatokea wanaume wengi kwa umbile la msichana mrembo mno.

Yako mengi sana, lakini kwa uchache ni haya mjukuu wangu, cha kufanya sasa ni moja tu, kumsaidia mwenzako."

"Tunamwokoaje sasa mzee?"

"Yaani hapo cha kufanya ni kuongea naye ili tufanye utaratibu wa kumtoa mdudu huyu. Atamtesa sana kwenye maisha yake. Hatoolewa kwenye maisha yake hata kama wewe baadaye ukiamua kutaka kumuoa, huwezi."

"Unajua mimi naogopa sana mzee Raia hata kuendelea naye!"

"Hapana kijana, kama nilivyokwambia, yule jini alipanda kwa sababu ya ile harufu ya udi, kwa hiyo tahadhari kama utaendelea naye usiwashe kitu chochote kinachoitwa udi chumbani kwao, au manukato makali siku anapokuja. Au wenyewe mwenyewe usipake pafyumu yenye harufu inayofanana na udi.

Hii itakusaidia sana. Ila kikubwa zaidi tumsaidie huyu dada, sasa kwanza tumuulize, halafu tujue la kufanya."

Heri aliona ni jambo jema kwa sababu kama Nuru atakubali hilo, akasaidiwa na kupona, hata yeye mwenyewe itampa sifa kwake na familia ya msichana huyo.

Baada ya kuridhika na walichokiongea walitoka nje na kumkuta Nuru tayari akili zimeshamrudia kwa asilimia zote mia moja.

Alichoonekana nacho machoni ni




**"Ahsanteni sana wote, nashukuru sana kwa kupambana hadi kurudi kwenye hali hii. Nawapa pole kwa sababu sijui kama mlikuwa mnajua chochote kabla na mimi ni mara ya kwanza kufika hapa."**

uchovu na aibu tu. Akuwa amekaa pale pale alipokaa.

"Pole sana binti." Mzee Raia alimwambia kwa sauti ya upole. "Ahsante sana mzee." Akajibu kwa sauti ndogo ya uchovu na mikwaruzo.

"Pole Nuru, pole sana mama."

Heri naye akaongezea. Wakati huo woga wote ulikuwa umemuishia. Semina aliyopigwa ndani na mzee Raia ilimuingia kisawasawa na kuelewa kila kitu.

Alishajua kilichotokea ni ktu gani, nini kilisababisha, na kitu gani kifanyike baada ya hapo.

Wote wawili walikaa pembeni yake na kumfariji ili asijisikie unyonge.

Kitendo cha kupandishwa maruhani kwa mpenzi, tena siku ya kwanza tu tangu afike, na sehemu ambayo ni mbali na nyumbani kwao, ilimnyong'onyesha mno Nuru.

Ni kama mtu ambaye amewekewa siri zake zote nje.

Hakujua tena hatma yake, lakini aliombea mambo yaishi pale ili arudi nyumbani kwao na asirudi tena.

Hakutaka tena kurudi sehemu ambayo wameshamtambua yukoje, au kuwa na uhusiano na mwanaume ambaye amejua aibu yake.

Alikuwa pia na uhakika kuwa baada ya tukio lile tu, Heri hatokuwa na mapenzi naye.

Wakati mwingine mwanaume kuendelea kumpenda au kumvumilia mwanamke mwenye changamoto kadhaa ikiwemo kama hiyo, kuanguka kifafa, au matatizo mengine yanayofanana na hayo, ni ngumu sana.

"Ahsanteni sana wote, nashukuru sana kwa kupambana hadi kurudi kwenye hali hii.

Nawapa pole kwa sababu sijui kama mlikuwa mnajua chochote kabla na mimi ni mara ya kwanza kufika hapa."

"Huna sababu ya kutupa sisi pole, sisi ndiyo tukupe pole binti, huyu mwenzako ndiye alikuja kuniita baada ya kukuona haupo kwenye hali yako ya kawaida. Nilipofika kukuona tu, nilijua tatizo ni nini, ndiyo tukakuleta hapa tukalishughulikia, umerudi kwenye hali ya kawaida."

"Mzee nashukuru sana, wengine wanakuwa hawajui, basi mateso wanakuwa makubwa sana."

"Mimi ni mtu mzima, na kwa bahati nzuri najua sana mambo haya vizuri tu. Ila kuna vitu siku nyingine nataka kukuuliza ili tulimalize ili tatizo kama utapenda."

"Kwa nini mzee unasema kama nitapenda?"

"Ndiyo maana wengine hawataki maruhani yao yatoke kwa sababu mbalimbali, wengine huwa yanawalinda, wengine yanawapiga mkwara ili mradi tu."

"Mzee mimi ni msichana mdogo sana, wala sipendi haya madudu, yameniingia mimi mwenyewe nikiwa sijui. Na aliyesababisha haya yote ni mama wa kambo, hakuwa mtu mzuri kabisa..."

"Basi basi mama, leo usiongee sana maana bado hauko kwenye hali ya kawaida, unabidi ukapumzike nyumbani, ila baada ya wiki moja urudi hapa ili tulimalize hili tatizo."

"Yaani mzee kama unaweza kulimaliza mimi nitashukuru sana, maana rafiki zangu wameshawahi kunipeleka maeneo tofauti lakini imeshindikana. Mimi siitaki hali hii, nataka niwe mzima kabisa."

"Nitaliondoka hilo tatizo, tena bure, sitaki hata pesa yako, huyu mwenzako ni rafiki yangu sana, huwa tunakutaka njiani na tunaongea sana, ingawa nilikuwa sijawahi kufika kwake na yeye kwangu, leo hii alifika kwa sababu alinihitaji."

"Nashukuru sana mzee Rais kwa yote uliyoyafanya, nadhani sasa uende ukapumzike tu, mimi niache nimsindikize bibie huyu kituoni..." "Hapana kijana, hu inafaa amkodoshie bajaj, impeleke hadi kwao, siyo tena wa kwenda kuparamia mabasi, ashuke halafu aomgoze hadi nyumbani, au kupanda bodaboda kwa sababu anaweza kupata kizunguzungu. Ni wa kumkodishia bajaj." Akashauri mzee Raia. Ukaungwa mkono na Heri.

"Vipi uko vizuri?" Akauliza Heri wakati anampandisha bajaj. "Ndiyo ila kichwa tu ndiyo bado kinaniuma sana."

"Pole, ngoja nikupeleka mpaka pale Chanika mwisho, nitashuka, nitakuacha ikupepeke nyumbani."

"Ahsante sana." Kwa upande wa Nuru alianza kuona kama yupo sehemu sahihi. Kupata tatizo lile alilonalo hakufikiria kama angepewa huduma nzuri vile, kufarijiwa na watu ambao ni mara ya kwanza kwenda kwao, kukukutana na tatizo lile, kulitatua na kuahidi kulimaliza kabisa. Hakuona unyanyapaa wowote kwake. Walionekana kumsaidia kwa hali na mali.

Mpaka anateremka aliendelea kuona upendo ule ule kwa Heri. Hiyo ilimtia moyo sana.

Akajiambia moyoni kuwa atarejea tena ili aone mwisho wake. Safari hii atarejea akiwa na nia ya kwenda kuelezea sababu ya yeye kutupiwa jini alilonalo, na ikiwezekana mzee Raia amsaidie kwa jinsi atakavyoweza.

ITAENDELEA JUMAPILI

# KIZZ DANIEL AMPA TUZO MKEWE


MWANAMUZIKI maarufu wa Nigeria, Kizz Daniel ameamua kumsifia mke wake kwa kumtungia wimbo maalum unaoitwa 'Double' ambao ameutambulisha jana.

Katika video ya wimbo huo, amemtumia mkewe kwa kuipamba kama ishara kwamba anamuamini na kumfanya rafiki yake hata katika kazi yake ya muziki.

Wimbo wa 'Double' unaonyesha mchanganyiko maridadi wa miondoko ya Afrobeat na kwaya na kusababisha ladha ya kipekee katika burudani.

Wimbo huu unafuatia mfululizo wa nyimbo kali alizotoa mwaka huu kama 'Twe Twe', 'Showa' na 'Too Busy to be Bae'.





# EMINEM ANAKUJA UPYA KUWASHIKA

RAPA mkongwe kutoka Marekani, Eminem amesema Albam yake mpya The Death of Slim Shady' itakuwa ya moto kutokana na nyimbo kali zilizokuwemo ndani.

Katika kuthibitisha maneno yake, Eminem, juzi alizindua wimbo wake mpya "Houdini" ambao ni wa kwanza kutambulisha kutoka kwenye albam hiyo.

Katika ukurasa wake wa Instagram, ametania kuwa atafanya kila uchawi kuhakikisha kazi zake zinakwenda sawa kama alivyopanga.

Hata hivyo, tarehe ya kutolewa kwa albamu imepangwa kuwa katika msimu huu wa joto.

Msanii mwenzake Dk. Dre alithibitisha kwamba Albam hiyo itakuwa kali kutokana na kuchangia nyimbo kadhaa kwenye mradi huo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CASEMIRO AGOMBEWA SAUDIA

KLABU kadhaa za Ligi Kuu ya Saudia (Saudi Pro), ikiwamo Al Nassr, Al Ahli na Al Qasidiya, zinawania kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 32 akitokea Manchester United msimu huu. (**Goal**)

### BRUNO KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham imefikia makubaliano ya mkataba wa pauni milioni 15 na Flamengo kwa ajili ya kumnunua mlinzi wa Brazil, Fabricio Bruno, mwenye umri wa miaka 28. (**Guardian**)

### MASON KUREJEA GETAFE

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Mason Greenwood, anataka kurejea katika Klabu ya Getafe msimu ujao baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 hivi majuzi kucheza mechi yake ya mwisho kama mchezaji wa mkopo katika timu hiyo ya La Liga. (**TEAMtalk**)

### VILLA, PALACE VITANI

KLABU ya Aston Villa na Crystal Palace zote za England zinatazamia kumnunua beki wa Gent, Archie Brown, mwenye umri wa miaka 22. (**Mirror**)

### BARCA KUMREJESHA FELIX

MABOSI wa Barcelona huenda wakamrejesha kwenye Uwanja wa Nou Camp kwa mara ya pili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix, kutoka Atletico Madrid. (**Sport**)

### ADARABIOYO ATAJWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inashinikiza kupata jibu kuhusu uwezekano wa kumnunua beki wa England, Tosin Adarabioyo, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 akitarajiwa kuondoka Fulham msimu huu wa joto baada ya mkataba wake utakapomalizika. (**Talksport**)

### VAN DEN BERG AGOMBEWA

LIVERPOOL imeeweka thamani ya pauni milioni 20 kwa mlinzi wa Uholanzi, Sepp van den Berg, mwenye umri wa miaka 22, ambaye ananyatiwa na klabu za Brentford, Southampton na Wolfsburg baada ya kung'aa alipokuwa kwa mkopo Mainz nchini Ujerumani. (**Athletic**)

### NAPOLI YAIBANIA PSG

NAPOLI imesema haina nia ya kumuuza winga wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, mwenye umri wa miaka 23 kwa Paris St-Germain, huku Antonio Conte akitarajiwa kuwa kocha wao mkuu mpya. (**Corriere dello Sport**)

### RODRYGO NJIA PANDA

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Brazil, Rodrygo, mwenye umri wa miaka 23, ametilia shaka mustakabali wake katika klabu hiyo, na hivyo kuongeza uwezekano wa kuhamia Liverpool. (**Mundo Deportivo**)

### OLMO AWA LULU ULAYA

KINYANG'ANYIRO cha kumsaka mshambuliaji wa RB Leipzig na Hispania, Dani Olmo, kimeshika kasi huku Barcelona, Manchester United, Manchester City, Liverpool na Bayern Munich zikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (Mundo Deportivo)

### CLARKE SOKONI ENGLAND

KLABU ya Southampton inawania saini ya winga wa Sunderland, Jack Clarke, ambaye ana umri wa miaka 23. (**Telegraph**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AMWAGA CHOZI

**JEDDAH,** Saudi Arabia

## Ni baada ya kumaliza msimu bila kombe lolote huku...

CRISTIANO Ronaldo alimwaga machozi baada ya timu yake ya Al Nassr kupoteza mechi ya Fainali ya Kombe la Mfalme wa Saudia dhidi ya Al Hilal iliyochezwa juzi na kumaliza msimu bila taji lolote.

**Al Hilal walishinda penalti 5-4 na kukamilisha ligi na makombe mawili baada ya mechi ya mjini Jeddah kuisha kwa sare ya bao 1-1 katika muda wa kawaida na wa ziada kushindwa kutoa mshindi.**

Kufuatia kushindwa kwa Al Nassr, Ronaldo alizama dimbani na hakufarijika huku wachezaji wenzake na wakufunzi wakijaribu kumfariji.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or hatimaye alitolewa nje ya uwanja lakini aliendelea kuzidiwa na hisia alipoketi kando kabla ya kupokea medali yake ya washindi wa pili.

Kupoteza huko kunakamilisha msimu wa kutatanisha kwa Ronaldo.

Al Nassr walimaliza katika nafasi ya pili kwa Al Hilal katika Ligi Kuu ya Saudia na kufungwa katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa wa Asia.

Februari Ronaldo alifungiwa kwa kuonyesha ishara ya matusi kwa mashabiki wa Al Shabab waliokuwa wakiimba jina la Lionel Messi, mpinzani wa muda mrefu wa mshambuliaji huyo.

Lakini Ronaldo mwenye umri wa miaka 39 alipata sifa nyingi za kibinafsi.

Katika msimu wake wa kwanza kamili wa Saudia, fowadi huyo wa Ureno alifunga mabao 35 yaliyovunja rekodi.

Lakini hakuweza kufanya lolote kuzuia timu yake kushindwa hapo juzi, licha ya kuzifumania nyavu wakati wa kupiga penalti.

Aleksandar Mitrovic aliifungia Al Hilal bao la kuongoza dakika ya saba kabla ya Aiman Yahya kupeleka mchezo huo hadi dakika za nyongeza kwa bao la kusawazisha dakika ya 88.

Pambano hilo lilishuhudia mwamuzi akitoa kadi tatu nyekundu, huku David Ospina akitolewa nje kwa kadi nyekundu kwa Al Nassr dakika ya 57 kabla ya Ali Al-Bulayhi na Kalidou Koulibaly kumfuata.

Kipa wa Al Hilal, Yassine Bounou, hatimaye alikuwa shujaa alipookoa penalti mbili za mwisho za Al Nassr na kutwaa taji hilo.

Mafanikio ya Al Hilal yamekuja licha ya fowadi nyota wa Brazil, Neymar kukosa takriban msimu mzima baada ya kuumia.

HABARI MICHEZO

# FERNANDES KIZUNGUMKUTI MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

WAKALA wa kiungo wa kati wa Manchester United, Bruno Fernandes, anaripotiwa kufanya mazungumzo na timu kadhaa za juu huku akijiandaa kuchukua uamuzi kuhusu mustakabali wa nyota huyo ndani ya klabu hiyo.

Ripoti za mabadiliko ya kikosi cha watu wengi za Aprili zilizua uvumi mkubwa kuhusu hatima ya Fernandes na United huku akikaribia miaka miwili ya mwisho ya mkataba wake, ambayo inajumuisha chaguo la miezi 12 zaidi.

Fernandes amesisitiza mara kwa mara nia yake ya kubaki United, huku pia akikubali hitaji lake la kuhisi kuthaminiwa na wale wanaosimamia.

Zaidi ya kuchochea moto wa kuondoka majira ya joto, Fabrizio Romano, alienda kwenye mtandao wa kijamii kufichua wakala wa Fernandes, Miguel Pinho, hivi karibuni amefanya mazungumzo na klabu mbalimbali za Ulaya.

Inadaiwa Fernandes bado anajitolea kwa United lakini pia bado hajafanya uamuzi wa mwisho juu ya kuendelea kwake Old Trafford.

Ingawa hamu ya Fernandes ya kusalia iko wazi, kisicho na uhakika ni hisia kwake kutoka kwa Sir Jim Ratcliffe na INEOS.

Mmiliki huyo mpya yuko tayari ameweka kikomo bajeti ya uhamisho wa majira ya kiangazi na kuhimiza United kukusanya fedha kupitia mauzo ya wachezaji, huku Fernandes akiwa mmoja wa mali ya thamani zaidi katika kikosi cha sasa.

Kocha Erik ten Hag amesisitiza anatarajia Fernandes kusalia msimu huu wa joto, lakini pia kuna shaka kuhusu mustakabali wa Mholanzi huyo huku Ratcliffe akijiandaa kufanya mapitio ya nafasi yake.

Ripoti kabla ya fainali ya Kombe la FA zilidokeza United walikuwa tayari wameamua kuachana na Ten Hag, ambaye ushindi wake kwenye Uwanja wa Wembley baadaye ulizua ripoti bosi huyo anaweza kubakishwa kwa kampeni zijazo.

# City yavutiwa na Rodrygo

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City imeripotiwa imeonyesha nia ya kumpa Rodrygo njia ya kuondoka Real Madrid iwapo hatafurahishwa na nafasi yake katika klabu hiyo.

Madrid wanajiandaa kutangaza kuwasili kwa Kylian Mbappe, ambaye wengi wanaamini atachukua nafasi ya Rodrygo katika safu ya ushambuliaji ya wachezaji wawili ya Kocha, Carlo Ancelotti.

Rodrygo hivi majuzi alikuwa na wasiwasi na mashabiki alipokataa mara mbili kuondoa uwezekano wa kuihama klabu hiyo.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca hali ya Rodrygo imevutia macho ya mabingwa wa Ligi Kuu England, Man City, ambao wako tayari kumpa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 nafasi ya kuondoka Madrid ikiwa hajisikii kama mshiriki wa kuthaminiwa wa kikosi cha kwanza.

City wanapanga kufuatilia hali hiyo na kama Rodrygo atajikuta nje ya kikosi cha Madrid, wakaambapo watakuwa tayari kuzindua ofa.

Hivi majuzi Liverpool walitajwa pia wanahitaji huduma ya nyota huyo.

Inasisitizwa Rodrygo bado anafuraha na Madrid na hataki kuondoka, ingawa ripoti za hivi majuzi zimekiri atazingatia chaguo lake.

Madrid hawataki kumpoteza Rodrygo na iliripotiwa hivi majuzi wangekuwa tayari kubadilisha timu yao nzima ili kutoa nafasi kwa Mbrazil huyo.

Rodrygo bado ana miaka minne kumaliza mkataba wake na hivyo maofisa wa Madrid hawana wasiwasi kuhusu mustakabali wake, wakiwa salama kwa kujua mchezaji huyo hatazamii kuondoka klabuni hapo.




# Maatsen njia panda Chelsea

**LONDON,** England

SITOFAHAMU ya wapi atakapocheza beki wa kushoto wa Chelsea, Ian Maatsen, imeibuka huku akicheza mechi ya mwisho ya Fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Borussia Dortmund anayoitumikia kwa mkopo.

Maatsen imeibuliwa na Gazeti la Daily Mail, ambalo limeandika beki huyo wa kushoto kutoka nchini Uholanzi bado hajaamua ni wapi anataka kucheza msimu ujao 2024/25.

Gazeti hilo limeripoti Maatsen bado hajaamua juu ya mustakabali wake na Chelsea licha ya kusaini mkataba wa hadi Januari, mwaka 2026, huku Borussia Dortmund ikiwa na nia ya kuendelea kumtumia kwa kumsajili moja kwa moja, ikitarajia kumia kipengele cha mkataba wake, ambacho kinaruhusu beki huyo kuuzwa kwa pauni milioni 35.

Maatsen, ambaye ni zao la Akademi ya Chelsea, kwa sasa yuko Dortmund kwa mkopo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alianza mchezo mmoja pekee wa Ligi Kuu mwanzoni mwa msimu huu, kabla ya kutimkia Ujerumani Januari, 2024, ambako amekuwa akianza mara kwa mara na kucheza kila dakika ya mechi zao za mtoano za Ligi ya Mabingwa.

"Hata hivyo Kocha mpya wa Chelsea, Enzo Maresca, anatazamwa kama suluhisho la Maatsen kurudi klabuni hapo ama kusalia jumla Dortmund.

Hata hivyo Chelsea haina changamoto ya beki wa kushoto, kwani kwa sasa inao Marc Cucurella na Ben Chilwell.



HABARI MICHEZO

# STARS, INDONESIA KATIKA MAJARIBU MUHIMU LEO

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) inatarajiwa kuvaana na wenyeji Indonesia katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa leo kuanzia saa 6:00 mchana (saa za Tanzania), kwenye Uwanja wa GBK Madya jijini, Jakarta.

Stars inacheza mechi hiyo ili kujiandaa na mchezo wa kufuzu Fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Zambia utakaopigwa Juni 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa, jijini Ndola.

Kocha wa Stars, Hemed Morocco, amesema baadhi ya wachezaji ambao hawakuwamo awali safarini, tayari amewasili Jakarta, na ana uhakika mechi hiyo itakuwa ni kipimo sahihi kwa kikosi chake.

"Maandalizi yapo vizuri, kwa sasa tumetimia maana kuna nyota wengine wameshajiunga na timu huku, tumefanya mazoezi vizuri tu, kuna marekebisho madogo madogo tunajaribu kuyatatua ndani ya kikosi chetu, wachezaji wote wapo katika afya njema, tunatumaini tutapata matokeo mazuri kwenye mchezo huu," alisema Morocco.

Naye mchezaji wa timu hiyo, Himid Mao, alisema amefurahi kupata muda wa kufanya mazoezi kwa pamoja, baada ya kuwasili kwa mafungu, hivyo ana imani watafanya vyema.

"Nafikiri kila kitu kiko sawa, tumejiandaa na tumetimia, tumepata nafasi ya kucheza mazoezi kwa pamoja wachezaji wote angalau mara moja, licha ya kuwasili kwa nyakati tofauti," Mao alisema.

Tanzania ipo katika Kundi E, ikishika nafasi ya nne ikiwa na pointi tatu kwa mechi mbili ilizocheza, sawa na vinara Morocco, Zambia na Niger, huku yenyewe ikiwa nafasi hiyo kwa tofauti na mabao ya kufunga na kufungwa.

Hata hivyo baadhi ya wachezaji nyota walioitwa na Morocco akiwamo mshambuliaji, Simon Msuva, wamegoma kuwa sehemu ya mechi hiyo kutokana na madai wanahitaji kupumzika baada ya kumaliza msimu.



Wachezaji wa mpira wa kikapu wa Timu ya Vijana wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa JKM Park jijini, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kampeni michuano Euro yaanza kutoa washindi

**Na Faustine Feliciane**

SIKU chache baada ya kuzinduliwa kwa Kampeni ya Michuano ya Ulaya 'Zigo la Euro 2024', tayari washindi wameanza kupatikana.

Michuano ya Euro 2024 inatarajiwa kuanza hivi karibuni nchini Ujerumani, na baadhi ya mashabiki watapata fursa ya kwenda kushuhudia michuano hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa Wateja wa Maalum wa Tigo Pesa, Mary Ruta, alisema katika kampeni hiyo watatoa zawadi mbalimbali ikiwamo safari ya kwenda kushuhudia michuano hiyo.

Ruta alisema washindi hao wanaingia katika droo kwa kufanya miamala au kushiriki mechi kupitia Parimatch.

"Leo (jana) tumepata washindi wa kwanza ambao wamejishindia zawadi mbalimbali.

Alisema washindi hao wamepata zawadi ya jokofu, televisheni, fedha na tiketi moja ya kwenda kushuhudia michuano hiyo.

Aliwataja washindi hao ni pamoja na Maurin Shirima ambaye alijishindia televisheni, Ramadhan Mrutu, amepata tiketi ya kwenda Ujerumani huku zawadi ya Sh. milioni moja ikienda kwa Fredy Mlay.

## Gamondi: Hatutarudia..

INATOKA UK. 24

Kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Feisal Salum 'Fei Toto' alisema wamejiandaa kutoa burudani kwa mashabiki wao na wamejipanga kupambana ili kutwaa ubingwa wa michuano hii kwa msimu huu.

Fei Toto alisema watafuta maelekezo yote ya mwalimu wao hasa katika suala la kucheza kwa utulivu 'mkubwa' na bila ya hofu ya mchezo.

"Tunawaheshimu wapinzani wetu, na tunajua tunaenda kucheza na timu nzuri iliyo na wachezaji wazuri ambao malengo yetu ni moja katika kushinda mchezo huu.

Kwangu utakuwa mchezo mzuri, nacheza kwenye ardhi ya nyumbani, tumejiandaa vyema na Insha Allah tutafanya kile tulichokifanya katika mechi ya mwisho kukutana," alisema Fei Toto.

Beki wa kati wa Yanga, Ibrahim Baca, alisema wapo tayari kwa mchezo na wanawajua vizuri wachezaji wa Azam.

"Ni mchezo mzuri, Azam ni timu nzuri msimu huu, lakini sisi kama wachezaji tupo tayari kupambana, nina uhakika kila mchezaji atakayepata nafasi ya kucheza ataipambania timu," alisema Baca.

Aliongeza wachezaji wote wako tayari kwa mchezo huo na wamejipanga kufuata maelekezo yote ya kocha wao ili kuhakikisha wanatetea pia taji hilo.

## Kagoma aichagua..

INATOKA UK. 24

Simba wanavyocheza, wale siyo namba sita, ni nane, wanalazimika kwa sababu hakuna mwenye namba halisi," kilisema chanzo hicho ndani ya Singida Fountain Gate.

Kama Simba itafanikiwa kumalizana na mchezaji huyo, atakuwa wa pili kwa wachezaji wa ndani, baada ya kuwapo kwa taarifa za kumnasa beki wa kati ya Coastal Union, Lameck Lawi.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kwa sasa wana watu ambao wametapakaa kila eneo la Afrika kusaka wachezaji bora, lakini pia wanaangalia wachezaji wa ndani wenye hadhi ya kuichezea timu hiyo ambao walifanya vyema katika Ligi Kuu msimu uliomalizika.

"Tumeshasema tutafanya usajili mkubwa mno, ila kwa sasa hatuwezi kuwataja ni nani atasajiliwa na nani ataachwa, mpaka pale muda wa kufanya hivyo utakapofika," Ahmed alisema.



# Michezo

Jumapili Juni 2, 2024

Nipashe




Ronaldo amwaga chozi UKURASA 21



Fei Toto

Aziz Ki

## Kagoma aichagua Simba

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA imedhamiria kuboresha kikosi chake kuelekea msimu mpya wa mashindano, Simba inatajwa imekaribia kumnasa kiungo mkabaji wa Singida Fountain Gate, Yusuph Kagoma, ambaye awali alitajwa yuko kwenye rada za mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga.

Habari kutoka ndani ya Singida Fountain Gate zinasema, Simba imeingia kati dili hilo, huku mchezaji mwenyewe pia akionekana kufurahia kujiunga na Wekundu wa Msimbazi ambako anaona ni rahisi zaidi kupata namba kwa sasa kuliko akitua Jangwani.

"Yanga ndiyo ilikuwa ya kwanza, ilileta ofa mambo yakawa mazuri na hata sisi tulijua anakwenda huko, ghafla upepo umebadilika, Simba wameingilia kati, ingawa ofa yao si kubwa sana, lakini mchezaji mwenyewe ameonyesha anapenda kwenda huko. Katuambia mwenyewe akienda Msimbazi ana uhakika moja kwa moja na namba," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza katika mazungumzo yao, Kagoma amewaambia endapo akienda Yanga kutakuwa na changamoto kidogo kwa sababu namba anayocheza yupo, Khalid Aucho, Mudathir Yahya, Jonas Mkude na Zawadi Mauya, hivyo kutakuwa na vita ya kupata nafasi ya kucheza ukilinganisha na Simba.

"Ndugu yangu mwandishi, Kagoma ni kiungo mkabaji mzuri sana, anakaba vizuri, hana rafu za ajabu ajabu kama walivyo viungo wengi wa aina hiyo, na Simba inakosa mtu mkabaji halisi pale kati kwa muda mrefu, yeye anajua hilo, anaona ni fursa ya kwenda kuingia moja kwa moja kwenye kikosi.

Pale kina Babacar Sarr, Sadio Kanoute na Mzamiru Yassin, hawawezi kumweka nje kwa sababu kama unalijua soka na unaangalia

INAENDELEA UK 23

# Gamondi: Hatutarudia makosa

## Kocha huyo aahidi kulipa kisasi FA, Fei Toto atamba watapiga...

**Faustine Feliciane na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HATUTARUDIA makosa, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, kuelekea mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC itakayochezwa leo kuanzia saa 2:15 usiku kwenye Uwanja wa New Amaan Complex ulioko visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gamondi alisema amewaandaa vyema wachezaji wake kuhakikisha hawafanyi makosa na hatimaye kuibuka na ushindi katika mechi hiyo muhimu.

Gamondi alisema wanaukumbuka mchezo wa mwisho timu hizo zilipokutana katika Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo kikosi chake kilipoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya wapinzani wao hao.

**"Tumejiandaa vizuri, kila kitu tumekimaliza, tunasubiri mchezo, hautakuwa mchezo mwepesi kwa sababu Azam ni timu nzuri, mechi yetu ya mwisho kukutana nao tulipoteza, hatutaki hilo litokee tena," alisema Gamondi.**

Kocha huyo alisema wataingia uwanjani kwa tahadhari na watacheza mpira wao kwa umakini ili kuhakikisha wanapata ushindi na kubeba ubingwa.



"Malengo yetu ni kuchukua vikombe vyote msimu huu, tumefanikiwa kupata ubingwa wa Ligi Kuu, sasa tumebakisha Kombe la FA ili tukamilishe malengo yetu," alisema Gamondi.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam, Bruno Ferry, alisema amewaandaa wachezaji wake kuongeza umakini katika mchezo huo lakini pia kucheza kwa 'kuenjoy' na kutokuwa na papara ili kuhakikisha wanakamilisha mpango wao wa kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Ferry alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu Yanga imekuwa na timu yenye msimu mzuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo wachezaji wake wanatakiwa kuzidisha utulivu.

"Wachezaji wacheze kwa kuzingatia nini tunahitaji mwisho wa msimu huu, tumemaliza ligi tukiwa katika nafasi ya pili, hivyo tunahitaji kutwaa kombe hili, tunajua tunaenda kucheza na mabingwa wa ligi, hivyo suala la umakini linahitajika ili tufikie malengo," alisema kocha huyo.

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042